

# Maswali ya Maisha





# Yaliyomo

1.	Yesu ni nani?	Ukurasa 5
2.	Kwa nini Yesu alikufa msalabani?	Ukurasa 12
3.	Nitakuwaje na hakika juu ya Imani yangu?	Ukurasa 18
4.	Kwa nini nisome Biblia? Niisomeje?	Ukurasa 22
5.	Kwa nini nisali? Nisalije?	Ukurasa 28
6.	Roho Mtakatifu ni nani?	Ukurasa 34
7.	Nawezaje kushinda uovu?	Ukurasa 41
8.	Mungu anatuongozaje?	Ukurasa 47
9.	Kwa nini tuwaambie wengine?	Ukurasa 52
10.	Je, Mungu anaponya leo?	Ukurasa 57
11.	Kanisa ni nini?	Ukurasa 62
12.	Je, Naweza kuutumiaje vizuri muda wa maisha yangu uliobaki?	Ukurasa 68

a

Masomo haya yamejengwa katika msingi wa kozi ya 'Alpha' iliyoandikwa na Nicky Gumbel, Kasisi wa Kanisa la Utatu Utakatifu, Brompton, London, na hasa katika kitabu chake 'Questions of Life' Namshukuru sana kwa ruhusa yake kutumia kitabu hicho kuwa msingi wa kitabu hiki.

Nawashukuru sana wale ambao wamenisaidia na kurekebisha Kiswahili changu ili kitabu hiki kiwe rahisi kuelewaka. Hasa nawashukuru Rev. Jacob Chimeledya na Bw. Patrokili Silayo kwa msaada wao mkubwa. Nawashukuru pia David Walker aliyechora picha, na David Eyre aliyefanya marekebisho kwenye komputa.

© Rachel Tarling, Mpwapwa, Tanzania

January 2000

## **Utangulizi**

Kitabu hiki kina lengo la kuwawezesha watu watazame msingi wa Imani ya Kikristo, na kukua katika Imani hiyo. Ni kwa wote, wale ambao wamekuwa wakristo tangu zamani, na pia wale wanaotaka kujifunza, lakini siyo wakristo, ili kuona kama kweli wanaweza kuamini.

Katika kila sura kuna sehemu ya mafundisho, na sehemu ya maswali. Si kama kitabu cha shule. Hakuna jibu moja lililo sahihi kwa kila swali. Maswali ni kama chombo cha kutuwezesha kujadili mafundisho na kuyatendea kazi katika maisha yetu. Tena, hakuna mtaalam anayeweza kufaulu pasipo wenzake. Kila mtu anaweza kujibu, na kujifunza, na kuyatumia kukuza katika Imani yake - kuanzia kasisi mpaka mtu yule ambaye hajawa Mkristo bado!

Kozi hii inafaulu zaidi ikiwa wote wanakutana pamoja kwa kipindi cha mafundisho, halafu watu wanagawiwa katika vikundi vidogo vya watu sita au wanane kwa majadiliano. Tena, vikundi vikiwa na watu wale wale kila mara, watu wanazoeana na kuaminiana, na kufungua mioyo kuliko vikundi vikiwa na watu tofauti kila mara. Tena majadiliano yabaki katika vikundi ili vikundi viwe mahali ambapo watu wanaweza kuuliza maswali na kueleza wazi matatizo yao, machungu na mashaka yao bila hofu.

## Yesu ni nani?

Katika sura hii, tutatazama swali - Yesu ni nani. Watu wamekuwa na mawazo mengi juu ya swali hili - ni mtu katika hadithi, ni nabii, ni mtu katika historia, ni mganga, ni bingwa wa mazingaombwe. Je, tunaweza kumwamini, au kumwamini ni kama kupoteza akili, kuamini kama kipofu? Katika wakati wa sasa, je, tunaweza kutumia sayansi kueleza mambo yote, au bado ni swali muhimu?

Kwanza, kweli aliihi, au ni hadithi tu? Hatuna mashaka kwamba aliihi kweli kwa sababu kuna mashahidi wengi walioandika kuhusu maisha yake, si katika Biblia tu, lakini katika barua na vitabu nya kipindi kile. Kwa mfano, Josephus, aliyeandika historia ya wakati ule, alimtaja.

Zaidi kuliko hii, maandishi ya Biblia ni halisi hata kuliko maandiko mengine tunayoyategemea kujua historia yetu ya kawaida. Kwa mfano, kitabu kuhusu vita ya Warumi kinachoitwa 'Livy's Roman History', tuna nakala za zamani kama ishirini, zilizotengenezwa miaka 900 baada ya Livy kuandika maandiko ya kwanza. Kwa Biblia, tuna nakala kama elfu kumi za zamani, zilizoandikwa yapata miaka 300 tu baada ya kuandikwa mara ya kwanza. Kwa hiyo wataalam wote wanakubali kwamba Biblia yetu ni kama ilivyoandikwa mwanzoni na maandishi yake - hajabadiilishwa tangu mwanzo.



Pili, hatuna mashaka kwamba Yesu alikuwa binadamu kama sisii. Alichoka (Yoh 4:6), alikuwa na njaa (Mat 4:2). Alikasirika (Mk 11:15 - 17), alipenda (Mk 10:21) alikuwa na huzuni (Yoh 11:35), alijifunza (Lk 2:52), alifanya kazi (Mk 6:3), aliwatii wazazi wake (Lk 2:51).

Lakini watu wengi leo wanasema kwamba Yesu alikuwa mwanadamu tu. Mwanadamu maalum, lakini mwanadamu tu. Mwalimu mzuri, lakini mwanadamu tu. Wakristo wanasema kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Tutatazama ushahidi unaoonyesha kwamba alikuwa zaidi kuliko mwanadamu wa kawaida.

## **Yesu alisemaje kujihusu?**

Ni kweli kwamba Yesu hakusema wazi ‘Mimi ni Mungu’ Lakini mafundisho yake yote na maneno yake yote yalionyesha kwamba alijija kuwa Mwana wa Mungu pekee. Mafundisho yake mengi ni kuhusu yeye mwenyewe. Kwa mfano, alisema watu wakiwa na njaa, waje kwake watashiba. (Yoh 6:35) Au tena Alisema kwamba kumwona yeye ni kama kumwona Mungu mwenyewe. (Yoh 8:12, Yoh 11:25 – 26)

Alionyesha kwamba alikuwa na uwezo kama Mungu. Kwa mfano, alisema kwamba anaweza kusamehe dhambi. Tazama Mk 2:5. Viongozi walisema ‘Mbona anasema hivyo? Nani anaweza kusamehe dhambi ila Mungu mwenyewe?’ Yesu alionyesha uwezo wake kusamehe kwa kuponya mtu mwenye kupooza.

Tena alisema kwamba atauhukumu ulimwengu mwishoni mwa historia. (Mat 25:31) Mataifa yote yatakusanya mbele yake, na atawahukumu watu wote. (Mat 25:40, 45) Kama mtu wa kawaida angesema hivyo, ungemcheka. Lakini Yesu alisema hivyo, na watu walimheshimu na kuamini.

Tena, (Mk 14:61 - 64). Yesu aliuawa na Wayahudi kwa sababu alisema kwamba yeye ni Mungu. Au tena Yoh 10:33. Maadui zake walielewa kabisa kwamba anajiita kuwa Mungu. Hii ni sababu iliyowakasirisha, na kutaka kumwua.

Tumeona kwamba Yesu alisema kwamba yeye ndiye Mwana wa Mungu.

### **Kama si kweli**

- ◆ Ama alijua kwamba alisema uwongo, na ni mtu mbaya sana.
- ◆ Ama, alifikiri kwamba ni kweli - alijidanganya na alikuwa na kichaa.

Au

- ◆ **Ni kweli.** Kweli yeye ni Mwana pekee wa Mungu

Lakini hatuna nafasi kusema ni mwalimu mzuri tu. Hajatuachia hiari hii.

# **Kuna ushahidi gani kuunga mkono aliyojasema?**

## **Mafundisho yake**

Watu wengi, wasiowakristo na wakristo, wanajua sana mafundisho na hadithi za Yesu. Sheria za nchi nyingi zinafuata maadili kama yale aliyoafundisha. Ingawa tunaweza kwenda kutembelea mwezi, kuponya watu wanaoumwa sana, kujua zaidi katika kila eneo la sayansi na teknologia, bado hakuna mtu anayeweza kutoa mafundisho muhimu zaidi kuliko yeye. Je, kweli ni kazi ya mtu ambaye ana kichaa, au mtu mbaya?

## **Matendo yake**

Yesu alisema kwamba miujiza yake ni ushahidi (Yoh 10:38) Alichukua chakula kidogo, na kuwalisha watu elfu tano (Mk 6:30 - 44). Alikemea na dhoruba na ilitulia (Mk 4:35 - 41), aliwaponya vipofu, vilema, hata waliokufa aliwafufua. Na pamoja na kazi hizi, alionyesha upendo kwa wale waliotengwa na jamii, kama makahaba, na wenye ukoma. Je, mtu mbaya au mwenye kichaa anaweza kufanya hivyo?



## **Tabia yake**

Watu wengi wanamheshimu Yesu kwa sababu ya tabia yake, hata wasio wakristo. Watu wa wakati wake walipenda sana kuwa naye - walimfuata sana na kumwalika kuja kwao mara nyingi. Alionyesha kijitawala, lakini siyo kujitia huruma; unyenyekevu lakini bila udhaifu; furaha lakini bila kuwachekesha wenzake; upendo lakini bila kuvumilia mabaya. Maadui zake hawakuweza kuona kwamba amekosa. Je, kweli ni tabia ya mtu mbaya au mwenye kichaa?

## **Kutimiza unabii**

Katika maisha yake, Yesu alitimiza unabii zaidi kuliko nabii 300, zilizoandikwa katika miaka 500 iliyopita na manabii mbalimbali. Labda unaweza kusema mtu mwenye akili kubwa anaweza kuhakikisha kwamba atatimiza unabii fulani, lakini mara nyingine hawezi kuwa na uhakika wa baadhi ya mambo. Kwa mfano mahali ambapo atazaliwa, au atakapozikwa - ni vigumu kupanga mwenyewe.

## **Kufufuka kwake**

Ushahidi muhimu kuliko wote ni kufufuka kwake. Huu ndiyo msingi wa Ukristo. Lakini, kuna ushahidi gani kwamba kweli kulitokea?


## **Hakuwemo kaburini**

Wengi wamejaribu kueleza kwa nini Yesu hakuwemo kaburini:-

### **1. Hakufa**

Watu wanasema kwamba labda alipoteza fahamu msalabani lakini baadaye alipona. Lakini alipigwa sana - kipigo cha kutosha kuwua watu wengi. Alipigiliwa misumari na kukaa msalabani kwa masaa sita. Je, bila msaada angeweza kufungua kaburi? Askari pia walikuwa na wajibu kuhakikisha kwamba kweli amekufa. Wangalishindwa, na angalitoroka wangaliuawa. Hivyo walihakikisha kwamba kweli amekufa. Na askari alipomchoma mkuki wake, ilitoka damu na maji (Yoh 19:34). Tunajua kwamba mtu akifa damu yake inaganda na kugawanyika damu nyekundu sehemu moja na maji yake sehemu nyingine. Ndivyo ilivyokuwa na damu ya Yesu. Tunaweza kujua kwamba kweli alikufa

### **2. Wanafunzi waliiba maiti.**



Kwanza, warumi waliweka walinzi kaburini. Ingalkuwa vigumu sana kuiba maiti. Lakini zaidi ya hayo, wanafunzi wake walikuwa na huzuni sana. Hawakuamini kwamba Yesu atafufuka. Walikuwa wamekata tamaa. Walitoroka na kujificha. Baadaye, waliteswa sana, waliuawa kwa sababu walisema kwamba Yesu alifufuka. Wasingaliweza kufanya hivyo wote kama walijua kwamba kweli waliiba maiti wao wenyewe.

### **3. Wezi waliiba maiti**

Tazama Yoh 20:1 - 9. Kaburi halikuwa tupu - mlikuwa na vitambaa vy a sanda na leso iliyokuwako kichwani pake. Kweli wezi wangalismama kufungua maiti badala ya kuiondoa haraka? Na walitumaini kupata faida gani katika kuiba maiti?

### **4. Watawala walitoa maiti**

Ingalikuwa hivyo, kwa nini hawakuonyesha maiti wanafunzi walipoanza kusema kwamba Yesu amefufuka? Kwa nini waliona aibu? Je, ni kwa sababu hawakuweza kuonyesha maiti?

### **Yesu alikuwapo na wanafunzi**

Labda ilikuwa ndoto. Wanafunzi walijidanganya?

Wanafunzi walikuwa wavuvi, wafanyakazi, wenye afya. Sidhani kwamba wangaliweza kujidanganya. Pia, watu zaidi ya mia tano walimwona pamoja. Wanafunzi walimwona mara 10, katika kipindi cha wiki 6. Yesu aliweza kupika, kula, kuwafundisha. Haiwezekani kwamba ilikuwa ni ndoto.

### **Mwanzo wa kanisa**

Mara moja kikundi hiki cha wanafunzi kilibadilishwa. Walifundisha hekaluni na watu wengi wa kipindi kile waliamini. Katika kipindi cha miaka 300 tu, Injili ilihubiriwa katika ulimwengu wote.

### **Kanisa la sasa**

Ukienda kanisani leo, utakutana na watu wengi wanaosema 'namfahamu Yesu - si kama historia lakini kama mtu'. Ni watu wa kila aina, kila rangi, kila taifa, Walimu na wakulima, madaktari na wamaskini. Wote wanaweza kutoa ushuhuda kwamba Yesu anaishi.

### **Tumeona ushahidi kuhusu Yesu.**

Unaweza kusema - ni mtu mbaya au ni mtu kichaa. Lakini usiseme hivyo bila kuona ushahidi huu wa leo.

Unaweza kusema Kweli ni Mwana wa Mungu. Unaweza kusema 'Naamini; nisaidie kutokuamini kwangu'

Lakini huwezi kusema - Ni mwalimu mzuri, ni mtu wa historia, ni nabii wa kawaada. Haiwezekani

## Maswali

1. Utamjibu nini mtu anayesema ‘Siwezi kuwa Mkristo, lakini nafikiri Yesu alikuwa mtu mzuri sana’?
  2. Tunawezaje kupima neno la Yesu kwamba ni Mwana wa Mungu? Kwa nini unaamini /huamini kwamba ni kweli?
  3. Kwa nini kufufuka kwake Yesu ni msingi wa Imani ya Kikristo? Unafikiri nini kuhusu ushuhuda wa matukio haya?
  4. Ikiwa Yesu ni Mwana wa Mungu, inakuletea matokeo gani katika maisha yako?

## Ambatanisho

Yesu alisemaje kuhusu yeye mwenyewe?

### a. Mafundisho yake yaliyomhusu

- Mimi ni mkate wa Uzima (Yoh 6:35)
- Mimi ni nuru ya ulimwengu (Yoh 8:12)
- Mimi ndimi ufufuo na uzima (Yoh 11:25 - 26)
- Mimi ni njia, ukweli na uzima (Yoh 14:6)
- Ufalme wangu (Luka 22:30)
- Njoni kwangu (Mt 11:28 - 29)
- Nifuate (Mk 1:17 n.k.)
- Mkinipokea mimi.....mwampokea Mungu (Mt 10:40)
- Mkinikaribisha.....mwamkaribisha Mungu (Mk 9:37)
- Mkiniona mimi mmemwona Mungu (Yoh 14:9)
- Kunipenda mimi ni zaidi ya kuwapenda wanadamu      (Mt 10:37, Luka 14:26)  
wengine

### b. Alivyosema kwa mafumbo

- Kusamehe dhambi (Mk 2:5)
- Kuhukumu ulimwengu (Mt 25:31 - 32)

### c. Alivyosema kwa wazi

- Masihi (Mk 14:61 - 62)
- Mwana wa Mungu (Mk 14:61)
- ‘...kabla ya Abraham, nilikuwepo’ (Yoh 8:58)
- ‘Bwana wangu na Mungu wangu’ (Yoh 20:28)
- ‘Mimi ni Mungu’ (Yoh 10:33)

# **Kwa nini Yesu alikufa msalabani?**

Utaona mahali pengi alama ya msalaba wa Kikristo - kanisani, kwenye vibao, katika nguo, hata watu wanavaa kama mkufu. Tumezoea kuuona. Wangevaa picha ya bunduki, au panga, tungeshangaa, lakini tunasahau kwamba msalaba pia ulikuwa njia mbaya ya kufisha watu. Hata warumi waliuondoa mwaka AD 315 kwa sababu waliuona kama wenyewe ukatili mno. Hata hivyo, tunatumia alama ya msalaba kama alama ya Imani ya Kikristo. Zaidi ya nusu ya Injili inahusu matukio ya msalaba na kufa kwake Yesu. Vitabu vingine vya Agano Jipyä vinatumia nafasi kubwa kueleza maana ya kufa kwake Yesu. Ibada ya Ushirika Mtakatifu hasa inatukumbusha na kushangilia matukio ya msalaba. Paulo alipokwenda Korintho, alisema ‘naliazimu nisijue neno lolote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibowi’ (1Kor 2:2) Viongozi wengi wanakumbukwa kwa sababu ya maisha yao - Yesu anakumbukwa hasa kwa sababu ya kufa kwake.

Kwa nini tunaona kufa kwake Yesu ni muhimu hivyo? Kwa nini ni msingi wa Imani ya Kikristo?

## **Hitaji kuu la Mwanadamu**

Pengine watu wanasema ‘ninafurahia maisha yangu. Naishi vizuri, najaribu kumtunza jirani yangu, mimi si mtu mbaya’ Lakini, kila mmoja wetu anafanya mambo ambayo anajua moyoni kwamba si vizuri. Paulo anasema ‘wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu’ (Rum 3:23) Tukijipambanisha na mwizi au mwuaji, labda tunaweza kusema kwamba sisi si watu wabaya. Lakini kanuni ya Mungu ni Yesu Kristo mwenyewe. Tukijipambanisha na Yesu, je, tunaweza kusema kwamba sisi si wabaya? Ingetangazwa kanisani kila wazo baya lako, kila tendo lisilo na haki, kila unapotamani mke wa mtu mwingine, nani angeweza kusimama na farahi?

Kwa sababu sisi sote ni wenyewe dhambi, labda unaweza kusema ‘haidhuru. Ni hali ya kawaida ya wanadamu.’ Lakini dhambi ina matokeo yake maishani mwetu yanayotuharibu.



## **1. Uchafu wa maisha**

Yesu alisema ‘Kimtokacho mtu ndicho kimiachio unajisi. Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya, ukorofi, hila, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu. Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi’ (Mk 7:20 - 23) Ni kama tunavaa nguo chafu kwenye sherehe - pengine hazina matope na madoa makubwa, lakini si safi, na hatuwezi kuzisafisha. Ni tabia yetu ya kuwa na uchafu ndani.

## **2. Nguvu ya dhambi**

Dhambi zetu zina nguvu kutupendelea. Yesu alisema ‘kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi’ (Yoh 8:34) Ni kama kuvuta bangi inaweza kukushika mpaka ukashindwa kuiacha. Unaweza kuwa hivyo na dhambi ya mawazo mabaya, uasherati, wizi, uzinzi, tamaa mbaya, ukorofi - mara ya kwanza tunajisikia vibaya. Lakini tukifanya tena na tena, tunaanza kuzoea. Mwishoni hatuwezi kujizuia. Tunashikwa kabisa na kushikamana.

## **3. Adhabu ya dhambi**


Sote tunatambua kwamba uadilifu una haki. Mtu akiiba, budi ali pe deni lake. Mtu akimwua jirani, asiachwe kuendelea bila adhabu. Lakini hii si kwa ajili ya makosa ya wengine tu - pia sisi tunastahili kuadhibiwa kwa makosa yetu. Biblia inasema kwamba Mungu ni jahi wetu, na hakuna mtu anayeweza kusimama safi mbele ya Mungu (Rum 2:16)

## **4. Dhambi inatenganisha**

Mwishoni, kwa sababu ya tabia yetu ya dhambi, hatufai kuishi mbinguni na Mungu. Kama angwaingiza watu mbinguni na makosa yao, tungepaharibu! Kwa hiyo, siku ya mwisho, tutatupwa nje ya mahali anapokuwa Mungu, na tutaishi bila yeche daima. Hata sasa hivi, dhambi zetu zinasababisha mgogoro katika yetu na Mungu - hatuwezi kusikia sauti yake vizuri au hata kumtambua tunapoendelea katika hali ya dhambi (Rum 6:23, Is 59:1 - 2)

Kwa hiyo, matokea ya dhambi zetu si jambo dogo. Yanaleta tatizo kubwa.

## Mungu amefanya nini?



Tumeona kwamba dhambi zina nguvu - hatuwezi kuijokoa wenyewe. Lakini habari njema ya Injili ni kwamba Mungu alituona na hali mbaya hiyo, na alikuja mwenyewe kurekebisha mambo. Alikuja mwenyewe kubeba adhabu ya dhambi zetu. 'Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti.....kwa kupigwa kwake, mliponywa' (1 Pet 2:24)

Yesu mwenyewe alibeba adhabu tulioistahili sisi. Alihaihiniwa na marafiki zake. Alipigwa na mjeledi wenyewe sehemu ya mifupa ya wanyama ili kupasua ngozi ya watu. Alidhihakiwa na kundi la maaskari, kufungwa macho na kupigwa tena, akavalishwa taji la miiba mikali. Akavuliwa nguo awe uchi, akapigwa misumari kumkaza msalabani, Akainuliwa ili atundikwe pale penye jua kali masaa mengi, hali akiwa na maumivu makali, na kiu, mpaka pole pole akafa! Na wakati ule ule, alijisikia

kama ameachwa na Mungu, baba yake wa ukaribu, kwa sababu dhambi zetu zilisababisha utengano kati yake Yesu na Mungu. Huu ni upendo kweli kweli - hakustahili hata adhabu ndogo, lakini aliibeba kwa ajili yetu sisi.

## Yapi yalitokana na msalaba?

Ungeweza kuandika kitabu kizima kuhusu matokeo ya msalaba, lakini tutatazama picha nne Biblia inazotumia kutoka katika maisha yetu ya kila siku, kutusaidia kuelewa maana yake


### 1. Mahakama ya sheria (Rum 5)

Ni kama jaji mmoja alikuwa na mwana mkorofi. Siku moja, mwanae aliletwa mbele ya jaji huyu mahakamani kwa sababu ameiba mazao ya jirani yake. Baba afanye nini? Alimpenda huyo mwanae, na alijua kwamba hakuwa na fedha kulipa fidia. Lakini hakuweza kumsamehe bila adhabu, kwa sababu ni jaji mwenye haki. Kwa hiyo aliweka fidia alioistahili, halafu alitelemka kutoka kwenye kiti chake cha hukumu, na kulipa fidia mwenyewe kwa niaba ya mwanae.

Hii si picha halisi kwa sababu, kwanza si kwamba tunastahili fidia tu, lakini kuuawa kwa ajili ya dhambi zetu. Tena, bei haijalipwa kwa fedha, lakini kwa kitu cha thamani sana - yaani maisha ya mwana wa jaji pekee, Yesu Kristo.

## **2. Sokoni (Rum 3:24)**

Kuwa na madeni si tatizo la nyakati hizi - limekuwepo tangu zamani. Siku za nyuma, ikiwa mtu alikuwa na deni kubwa kabisa ambalo hakuweza kulipa, aliweza kujiuza sokoni kama mtumwa. Kwa mfano, akiwa na deni la shilingi milioni nne, aliweza kujiuza kwa mtu mtajiri kwa bei hiyo hiyo, afanye kazi kwake bila mishahara mpaka mwisho wa maisha yake. Fedha ilitumika kulipa deni lake. Ni kama hivyo kwetu sisi. Sisi tuna deni kubwa ambalo hatuwezi kabisa kulipa. Mungu anasema 'Mimi nitalipa deni lako. Wewe uje kuishi kwangu - lakini si kama mtumwa. Utakuwa kama mwanangu kamili' Yesu amelipa fidia yetu, na anatupa nafasi nzuri kuwa wanawe. 'Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi.' (Mk 10:45)



## **3. Hekalu (Ebr 10)**

Katika Agano la Kale, kuna sheria kabisa kuhusu kusamehewa dhambi. Kulikuwa na kanuni ya dhabihu mbalimbali zilizoonyesha uzito wa dhambi, na mahitaji ya kusafishwa. Kwa mfano, kama mtu akikosa alihitaji kuchukua mnyama ambaye hakuwa na waa lolote. Aliweka mikono yake kichwani pa mnyama na kukiri makosa yake. Ni kama mnyama amepokea makosa ya mtu, halafu akachinjwa. Hii ilikuwa kama picha ya mambo yatakayotokea, kutusaidia kuelewa. Soma Ebr 10:1 - 3, 11 - 14. Yesu alikuwa hana waa lolote, na alikuwa dhabihu kamili ya kuondoa dhambi zetu mara moja na milele.

## **4. Nyumbani**

Tumeharibu urafiki wetu na Mungu kwa makosa yetu. Sisi ni kama mwana mpotevu (Prodigal son) Lk 15:11 - 32. Lakini kazi ya Yesu msalabani ililetu uwezekano wa upatanishi 'Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao' (2 Kor 5:19) Mgawanyo wa dhambi umeondolewa, na tunaweza kurudi nyumbani kwa Baba tena

Picha hizi si kamili peke yake, lakini zinatusaidia kuelewa kwa nini Yesu alikuwa msalabani. Lakini tunaweza kuelewa bila ya kupokea wokovu wake. Tunaweza kuona kwamba ni hadithi inayofaa kwa ulimwengu, lakini si kwetu sisi binafsi. Yesu anatualika kupokea ukweli huo miyoni mwetu

binafsi, na kupokea upatanisho huo sisi binafsi. Je, unaweza kuungana na Paulo na kusema "Mwana wa Mungu ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu. (Gal 2:20)?

Usipokuwa na hakika, kuna sala katika ukarasa 55. Unaweza kuitumia na kuipokea kama yako. Uchukue nafasi hii kupokea mwaliko wa Mungu kwako binafsi, na kumshukuru.

## **Maswali**

1. Kwa nini Biblia inasema kwamba kutenda dhambi yoyote ni kama kuvunja sheria nzima?
  
  
  
  
2. Matokeo ya dhambi ni nini? Je, unakubali? Umeona ukweli huu katika maisha yako?
  
  
  
  
3. Mungu alifanya nini kuhusu matokeo ya dhambi zetu? Unajuaje kwamba hii inahusu matokeo ya dhambi zako wewe?
  
  
  
  
4. Nini maana ya ‘kuhesabiwa haki’?
  
  
  
  
5. Ina maana gani kupata uhuru kutoka kwa nguvu ya dhambi? Je ni kweli kwamba nguvu ya dhambi kutushika imevunjika?
  
  
  
  
6. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anasema kwamba haiwezekani kwa damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi (Ebr 10:3). Kwa nini basi walifanya dhabihu katika wakati wa Agano la Kale?
  
  
  
  
7. Utamjibuje mtu anayesema kwamba Mungu anakosa haki kwa sababu alimuadhibu Yesu badala ya sisi?


# Nitakuwaje na hakika juu ya Imani yangu?

Tunaambiwa katika Wakorintho 5:17 'Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipyä. Ya kale yamepita; tazama! Yamekuwa mapya'

Tunapopokea msamaha wa Yesu, tunaingia urafiki mpya. Labda unaweza kutaja tarehe ambayo ulianza maisha haya mapya. Labda iliteke taratibu kwa kipindi kirefu, lakini sasa unaweza kusema kwa hakika 'mimi namfahamu Kristo. Sijui iliteke lini, lakini mimi sasa ni mtoto mpendwa wa Mungu'

Kama mzazi mzuri, Mungu anataka tuwe na hakika kuhusu uhusiano wetu na yeye, na nafasi yetu katika familia. Hataki tuwe kama mtoto anayehitaji kusema 'sijui leo kama Baba atanifukuza kwa sababu hanipendi' Anataka tuishi katika hali ya hakika. 'Nimewaandikia ninyi mambo haya ili mjiue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu'(1 Yoh 5:13)

Kama kigoda, uhakika wetu unasi mama juu ya miguu mitatu, usianguke kwa urahisi. Unasi mama juu ya kazi ya watu watatu wa Utatu Mtakatifu - Neno la Baba, Kazi ya Mwana, na ushuhuda wa Roho Mtakatifu



## 1. Neno la Baba

Sisi tunajua vizuri kwamba hisia zetu zinaweza kutudanganya. Zinategemea hali ya afya yetu, hali ya hewa, hali ya mazao, hali ya ndoa. Leo tunafurahi, kesho tutakuwa na huzuni ingawa hakuna kitu ambacho kimebadilika. Lakini tunategemea neno la Mungu, kama rubani anavyojifunza

kutegemea vyombo vyake kupimia kwa mfano usawa wake juu ya ardhi, au juu ni wapi, kuliko kutegemea hisia zake.

Kwa mfano, katika Ufunuo 3:20 Yesu anasema ‘Tazama, nasimama mlangoni nabisha; mtu akiisikia sauti yangu na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na ye ye pamoja nami.’ Tukimwalika Yesu kuwa mwokozi wetu, ataingia kwa hakika, na kukaa ndani. Si jambo la imani, ni jambo la hakika. Tena alisema ‘Mimi nipo pamoja nanyi siku zote’ (Mt 28:20). Kama rafiki, labda hutazungumza naye kila wakati mnapofanya kazi pamoja, lakini unajua kwamba yupo.

Tena, ametuahidi kwamba tutakuwa na uzima wa milele (Yoh 10:28) Uzima huu unaanza sasa hivi, katika maisha ya sasa ya huzuni, na kuendelea daima. Anatuahidi kwamba siku moja Yesu ataleta Mbingu mpya na nchi mpya (Ufu 21:1), kwamba sisi tulio katika Kristo tutakuwa pamoja na Bwana milele (1 Thes 4:17), Hakutakuwa na maumivu tena, wala huzuni, wala dhambi. Tutamwona Yesu uso kwa uso (1 Kor 13:12). Tutapewa miili mipyä (1 Kor 15) Tutakuwa na tabia mpya kama Yesu (1 Yoh 3:2) Hili si tumaini tu, lakini tumaini lenye hakika, kwa sababu tangu mwanzo Mungu hajashindwa katika ahadi yake yoyote, na ye ye ana uwezo na amekusudia kufanya kwa hakika mambo yote ambayo ameahidi.

## **2. Kazi ya Yesu**

Tumesema kwamba hakuna kitu chochote tunachoweza kufanya ili kuijokoa sisi wenyewe. Msamaha wa Mungu hauwezi kununuliwa - ndiyo sababu Yesu alikufa msalabani. Kungekuwa na njia nyininge. asingekufa. Tungeweza kuijokoa sisi, Yesu angelikufa bure.

Kwa hiyo, tunajua kwamba wokovu wetu hauwezi kuitegemea kazi yetu wenyewe, bali ni kipawa cha Mungu. ‘Kwa maana, mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu’ (Efe 2:8 - 9). Kwa hiyo, kwa sababu haitegemei sisi, na tunajua kwamba kazi ya Yesu imeshafanikiwa, tunaweza kuwa na hakika kwamba wokovu wetu una hakika.

Si kwamba tunapomwamini, hatazamii kazi ye yote kwetu. Tukimwamini kweli, tutajitahidi kumfuata, kumtii, kuishi maisha ya Kikristo. Lakini hii si kupata wokovu wetu - ni dalili kwamba tumeshaelewa kweli kipawa chake. Haya ni matokeo ya wokovu wetu, si jinsi ya kuupata.

## **3. Ushuhuda wa Roho Mtakatifu**

Mtu akiokoka, Roho Mtakatifu wa Mungu huja na kukaa ndani yake. (Rum 8:9) Anapokuja anaanza kuleta mabadiliko ndani yetu.

Kwanza, anabadilisha tabia yetu ili tufanane na Yesu. Roho Mtakatifu

anapoingia ndani, matunda haya yanaanza kukua ‘Tunda la roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi. (Gal 5:22 - 23) Matunda hayaoti katika siku moja tu - inaweza kuchukua muda mrefu. Lakini, tukikumbuka nyakati za nyuma, tunaanza kuona kwamba tumebadilika. Labda hatukasiriki kwa wepesi kama mwanzoni, au tunaweza kumwonyesha upendo mama mkwe wetu.

Na baada ya muda, tutaona pia kwamba uhusiano wetu umebadilika. Badala ya kusoma Biblia kama wajibu, tunaanza kuwa na hamu ya kufanya hivyo. Tunaanza kujishughulisha na wengine. Tunaona furaha katika kumwabudu Mungu, na hamu ya kukutana na Wakristo wenzetu.

Pili, analeta uhakika moyoni mwetu. ‘Kwa hiyo, hamkupokea tena roho ya utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanya wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani Baba. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na Roho zetu ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu’ (Rum 8:15 - 16)

Mabadiliko haya hayatatokea katika siku moja. Ni kama tukiwa na safari ya kuvuka lkweta. Hatutaona mabadiliko moja kwa moja, lakini tukiendelea na safari yetu, pole pole tutaona kwamba hali ya hewa imeshabadilika, na tunaanza kuwa na hakika kwamba kweli tunaelekeea ncha ya kaskasini au kusini!

Kwa hiyo, tumeona kwamba tunaweza kuwa na hakika kabisa kuhusu imani yetu - hii si kiburi, bali ni kwa sababu tunategemea ahadi ya Mungu, kazi ya Yesu ambaye ameshafanya, na kazi ya Roho Mtakatifu maishani mwetu. Ingekuwa hali halisi ya kila mkristo, itatubeba katika taabu ya maisha haya mpaka tufike mbinguni.

## **Maswali**

1. Urafiki na Mungu una maana gani kwako?
2. Je, ni kiburi au ufedhuli kusema kwamba tuna uzima wa milele?
3. Kwa nini tunategemea ahadi ya Biblia na si hisia zetu?
4. Utajibu nini mtu anayesema kwamba anajitahidi kuishi vizuri, na anatumaini kwamba Mungu atamruhusu kuingia atakapofika mbinguni?
5. Kazi ya Roho Mtakatifu inatusaidiaje kuwa na hakika kuhusu imani yetu? Umeona ukweli huo katika maisha yako?
6. Bado una mashaka kuhusu imani yako? Kwa nini? Msaada gani unapatikana katika sura hii?

# Kwa nini nisome Biblia? Niisomeje?

Je, Unasoma Biblia? Wapenda kufanya hivyo? Au wafikiri kwamba ni kitabu cha zamani na matumizi yake yamekwisha.

Mara nyingi, mtu akianza upya kukisoma, anakuta kwamba kitabu hiki kilichoandikwa miaka mingi iliyopita kinamshika kwa nguvu. Hawezi kukiacha. Katika Zaburi ya kwanza twasoma kuhusu mtu ambaye 'sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, na sheria yake huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki. Na kila alitendalo litafanikiwa' Sheria ya Bwana ndiyo impendezayo. Alikuwa na vitabu vitano vya kwanza vya Biblia tu, lakini ndivyo vimpendezavyo. Vilimvuta kwa nguvu. Je, tunajisikia hivyo? Nataka kutazama jinsi tuwezavyo kujifunza kupenda Biblia kama hivyo.

Lakini kwanza tutazame habari chache kuhusu kitabu hicho.

Kwanza, Biblia inapendwa na watu wote kupita vitabu vingine vyote. Hata siku hizi katika Uingereza, nakala za Biblia zinauzwa kupita vitabu vingine vyote kila mwezi, kila mwaka. Ingawa vitabu vya aina nyingi vinapatikana kwa urahisi, na watu wengi wameacha kumwamini Mungu, hata hivyo, idadi ya Biblia zinazouzwa inapita idadi ya vitabu vingine vyote.

Pili, Kuna ushuhuda zaidi kwa maandiko ya Biblia kuliko vitabu vingi vingine vya historia. Tunaamini kwamba maandishi tunayoyakuta ya babu zetu ni kweli maandishi yao ingawa yanaweza kuwa ya zamani sana; na tunategemea historia humo ndani kwa taarifa ya historia yetu. Lakini kwa Biblia, tuna nakala nyingi za zamani sana, na tena maandishi mengine ya wakati huo huo kutusaidia tujue kwamba kweli ni maandishi ya zamani, na yanasema kweli kuhusu historia inayoandikwa humo.

Tatu, Biblia ina nguvu kupita vitabu vingine vyote. Vitabu vingine vinaweza kubadilisha maisha ya mtu, lakini Biblia huwa inafanya hivyo kupita vitabu vyote. Watu wa kila kizazi, wa kila taifa, wa kila umri, wa kila hatua ya elimu, wa kila aina wamekuta kwamba wakisoma Biblia, maisha yao yanabadilika.


Kwa nini ina nguvu hivyo? Kwa nini inapendwa na watu kwa kiasi hiki?

Ni kwa sababu ni mazungumzo ya Mungu na watu wake. Hatuwezi kujua kuhusu Mungu ila Mungu mwenyewe atufahamishe. Mungu amejifunua katika nafsi yake Yesu Kristo. Amejifunua pia katika maandiko ya Biblia. Waraka wa pili wa Timotheo unasema 'Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kuwaonya watu makosa yao, na kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema' (2 Tim 3:16 – 17)

Biblia ni pumzi ya Mungu. Kweli imeandikwa kwa kutumia binadamu, lakini bado ni kazi ya Mungu. Mungu hakuandikisha maneno yake kwa kusema kama sauti masikioni mwa watu; bali alitumia uwezo, tabia na maneno ya watu wenyewe. Lakini roho na ukweli wake aliweka upekee kwenye ufahamu ya watu hawa ili waandike hasa ukweli wake kwenye maandiko haya maalum. Walikuwa wavuvi, madaktari, wakulima, manabii, wafalme, na waliandika historia, barua, mashairi, unabii. Lakini yote ni pumzi ya Mungu, ili katuonyesha Mungu mwenyewe.

Lakini, kwa sababu ya aina nyingi za maandishi, maandishi mengine ni vigumu kuelewa. Hata mtume Petro alisema kwamba katika barua za Paulo 'yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa'. Lakini, tukisoma yote kwa jumla, tutakuta kwamba Mungu kweli anazungumza nasi.

Kwa sababu ni neno lake Mungu, lazima liwe na mamlaka kwenye maisha yetu. Linatusaidia kujua ni nini tunachokiamini, na jinsi ya kutenda vema. Inatuambia kwa mfano, kuhusu Yesu na kifo chake msalabani, kuhusu dhambi, mateso, mbinguni, mafundisho kuhusu Roho Mtakatifu n.k. Inatuambia pia kuhusu maisha mazuri, kwa mfano kutokutana kimwili nje ya ndoa, kusamehe wengine ambao wametukosea, kuwatunza jirani zetu, kuwatii wazazi, kulea watoto vizuri. Sheria hii si kama sheria ya kawaida, bali shabaha yake ni kutuletea uhuru. Wengine wanaweza kusema 'Sitaki kufuata mafundisho ya Biblia. Naona afadhali nifanye nipayo. Siudhi watu wengine' Lakini kazi ya sheria ni kuleta uhuru. Ukipacheza mpira bila mwamuzi na bila kufuata sheria, wachezaji wataanza kubishana na kuumia kwa sababu hawawezi kucheza vizuri, hawajui mipaka, na utundu unaweza kutawala.



Mwamuzi na sheria vipo ili kuleta uhuru wa kucheza vizuri. Vivyo hivyo, sheria ya Mungu katika Biblia ipo ili kuleta uhuru wa kuishi vizuri. Biblia inasema 'usikutane na rafiki yako nje ya ndoa' si kwa sababu Mungu ni mkali na hapendi tuwe na anasa. Inasema hivyo kwa sababu Mungu anajua kwamba watu wataumia, labda mtoto atazaliwa bila upendo, inaweza kuharibu ndoa na furaha. Tukifua sheria ya Mungu, tutaweza kuishi kwa furaha jinsi Mungu alivyotuumba.

Lakini Biblia siyo sheria tu. Unaweza kuisoma Biblia vizuri sana, na kujifunza kwa bidii kuhusu sheria yake na kujua mafundisho yake juu ya kila kitu, lakini bado umekosa shabaha yake kweli ya Biblia. Mungu ameiandika kwa sababu anataka tumfahamu binafsi. Yesu aliwaambia mafarisayo 'Mwayachunguza maandiko kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima.' Shabaha ya Biblia ni kwamba tujue jinsi ya kuingia urafiki na Mungu katika Yesu Kristo. Ni kama tunaposoma kitabu, mwandishi mwenyewe anatoka katika kurasa, na anaeleza mambo yote pale ndani. Tunaposoma Biblia tunakutana na Yesu Kristo mwenyewe. Anaweza kuzungumza nasi miyoni, na kutushauri, kuleta amani na furaha hata wakati wa matatizo, na kubadilisha maisha yetu ili tufanane naye. Tunajifunza kutambua sauti yake na kumfahamu zaidi kila siku.

## **Basi, tutasomaje Biblia?**

Kwanza tunahitaji kufanya mpango. Tusipopanga hatutaanza kwa sababu sote tuna vitu vingi vya kufanya. Tunahitaji kupanga labda dakika kumi kila siku kusoma Biblia. Afadhalii kufanya hivi kuliko kupanga saa moja nzima, na kushindwa kufanya hata dakika moja. Baadaye tukitaka tunaweza kuongeza muda.

Ni vizuri pia kutafuta mahali panapofaa unapoweza kuwa peke yako bila watoto kuja kupiga kelele na wengine kusumbua. Watu wengi wanafikiri kwamba asubuhi na mapema ni wakati mzuri, kabla kazi ya siku haijaanza.

Kwanza umwombe Mungu azungumze nawe unaposoma neno lake. Halafu unasoma mistari michache ya Biblia. Ukianza tu, labda ni vizuri kuanza na Injili. Unaweza kupata vitabu vya kukusaidia kupanga masomo; vinapatikana kwenye maduka ya vitabu vya kikristo, au unaweza kupanga mwenyewe. Ni vizuri pia kuwa na daftari la kuandikia vitu unavyovijifunza.

## Unaposoma, ujiulize

1. Inasema nini?
2. Maana yake nini kwa yule aliyeandika na wale waliopokea mara ya kwanza? (labda utahitaji kufanya utafiti kidogo, kwenye vitabu, au kumwuliza mchungaji)
3. Maana yake nini kwangu na kwa familia yangu, majirani zangu, jamaa yangu? Huu ndio wakati Mungu anaweza kusema nasi kuhusu maisha yetu wenyewe, na kutuonyesha anavyotaka tubadilishe, kutuonya, kutufundisha, kututia moyo, au kutuonyesha upendo wake.

Mwisho, ni muhimu kufanya tunavyosoma. Si kuongeza ujuzi tu, lakini kubadilisha jinsi tunavyoishi na kufanya kazi. Waraka wa Yakobo unasema 'mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake kwenye kioo. Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo. Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo na uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.' Tukijiangalia kwenye kioo, bila kufikiri 'Je, ninahitaji kunawa uso, au kuondoa uchafu nyweleni, au kubadilisha nguo?'; au tukiona ni lazima kurekebisha, lakini tunashindwa kufanya hivyo, tunapoteza muda bure. Lakini tukirekebisha jinsi tunavyoonekana, tunafanya vema. Na hivyo pia tunaposoma Biblia. Tukisoma tu bila kuwa tayari kubadilika, tunapoteza muda bure. Lazima tusome na mioyo iliyo tayari kumsikiliza Mungu na kumtii.



## **Tukisoma hivyo, kuna matokeo gani?**

Tukumbuke mstari wetu kutoka katika Zaburi. Mtu anayependezwa na neno la Mungu 'atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake' Tutazaa matunda - matunda ya Roho Mtakatifu yaani 'upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi'. Hii italeta faida kwenye maisha yetu, na pia kwenye maisha ya wenzetu, familia yetu, majirani zetu na jamaa yetu.

Pili, 'jani lake halinyauki'. Sisi sote tutakuwa na wakati wa shida. Lakini kama tupo tayari, tutakuwa na akiba ya nguvu inayoweza kutusaidia. Tukiweka neno la Mungu miyoni kila siku, wakati wa matatizo, tutaweza kulikumbuka na kutiwa moyo. Tukisubiri mpaka wakati wa shida , halafu tukajaribu kuanza kusoma Biblia na kumwomba Mungu wakati huo, itakuwa vigumu. Labda inawezekana, lakini labda tutashindwa. Afadhalii kuweka mizizi mirefu wakati wa masika, ili wakati wa jua kali, mizizi idumu bila kukauka.

Tatu, Zaburi inasema 'kila alitendalo litafanikiwa'. Labda hatutapata fedha nyingi au mali nyingi, lakini katika uhusiano wetu na Mungu na wenzetu, na katika furaha na amani, tutafanikiwa kweli. Hivi vina thamani sana kuliko mali tu, na tutapata furaha kubwa katika maisha yetu ya Kikristo.

## **Maswali**

1. Biblia inakupendeza? Kwa nini / kwa nini haikupendezi?
2. Kwa nini Biblia ni tofauti kuliko vitabu vingine muhimu?
3. Je, tunaweza kuamini Biblia yote kama pumzi ya Mungu? Kuna matatizo yoyote? Tunawezaje kupata msaada kutatua matatizo haya?
4. Utamjibu nini mtu anayesema kwamba Biblia ni kitabu cha sheria kinachotunyima uhuru wetu?
5. Unakubali kwamba Biblia ni kama barua ya upendo? Tunawezaje kukutana na Mungu mwenyewe humo ndani? Umeshona hii katika maisha yako?
6. Utamshauri nini mtu anayetaka kusikia sauti ya Mungu kwa kusoma Biblia?

## Kwa nini nisali? Nisalije?

Ukiwa uliza majirani zako, utakuta kwamba watu wengi wana kawaida ya kusali. Wengi wanasali kila siku - yewezekana walifundishwa kufanya hivyo tangu utoto. Wameendelea na kawaida hii hata wanapokuwa watu wazima, lakini hawana hakika kwamba Mungu ni nani. Wengine wanasali wakati wa shida - labda wakiishiwa fedha, au mtoto akiumwa, au wanapoona hatari au wamefiwa.

Basi, sala ni nini? Kusali ni kuzungumza na Mungu. Ni urafiki na Mungu. Inawagusa watu wote wa Utatu.

Tunasali kwa Baba. Mungu anajiita Baba. Anataka kujulikana kama Baba yetu. Ni kweli kwamba Mungu ni mwenyezi, na mkubwa sana kuliko sisi, na tuisahau kumheshimu. Wazia kwamba wewe ni mtoto wa Rais. Ni vizuri kumheshimu, lakini nafikiri kwamba atakuwa na huzuni kama huji kwake kama mtoto wake pia. Vivyo hivyo, Mungu ametualika kuwa watoto wake, na kujenga urafiki wetu naye kwa kusali.

Lakini pia tuisahau kwamba ni 'Baba yetu aliye mbinguni' Ana nguvu ya kuumba mbingu na nchi. Mwezi wa nane, mwaka 1977 Wamerekani walirusha roketi kutoa taarifa kuhusu sayari yetu. Iliruka kwa kasi zaidi kuliko risasi ya bunduki, lakini ilichukua muda wa miaka 12 kufika sayari ya Neputni, maili 2,700 milioni kutoka duniani. Sasa, haitapita nyota nyingine kwa miaka 958,000 tena. Kuna nyota 100,000 milioni katika sehemu hiyo karibu na jua letu zinazofanana na jua letu. Mungu wetu aliumba hizi zote. Hii ndiyo nguvu yake.

Kwa hiyo, tunaposali tunazungumza na Mungu mwenye nguvu kabisa, lakini hata hivyo ametualika kuja kwake kama watoto wake.

Pili, tunasali katika Yesu Kristo. 'Kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kumkaribia Baba katika Roho mmoja' (Efe 2:18). Hatuna haki wenyewe ya kumkaribia Mungu ila kwa msamaha wa Yesu alipokufa msalabani. Yesu ndiye aliyeondoa mgogoro kati yetu na Mungu. Hii ndiyo sababu mara nyingi tunamaliza sala yetu na maneno 'Katika jina la Yesu Kristo'

Ukiona hundi, thamani yake haitegemei tu kiasi cha fedha kilichoandikwa, bali inategemea hata juu ya mtu aliyetia sahihi. Mimi nikiandika hundi ya Shillingi milioni kumi, itakuwa haina thamani kwa sababu benki itakataa kulipa. Lakini kama Waziri Mkuu ameandika hundi hiyo hiyo, itakuwa na thamani sana, kwa sababu ana fedha ya kutosha kulipa. Tunapoomba katika jina la Yesu Kristo, maombi yetu hayategemei akiba yetu mbinguni, bali haki yake Yesu Kristo isiyo na mwisho.



Tatu, tunasali kwa msaada wa Roho Mtakatifu. 'Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo; lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. Na ye ye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu' (Rum 8:26 - 27) Roho Mtakatifu anatusaidia tujue miyoni jinsi ya kuomba vizuri. Tutajifunza zaidi kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu katika somo lingine.

## **Kwa nini tuombe?**

Kuna sababu nyingi. Kwanza ni njia ya kujenga uhusiano wetu na Mungu. Huwezi kuwa na urafiki bila ya kuzungumza. Kusali siyo kuomba kwa mahitaji tu. Ni mazungumzo kuhusu kila kitu. Ungekuwa na rafiki anayekuja kwako wakati wa shida yake tu, kuomba msaada, ungefikiri 'Ni urafiki gani huu?' Bali marafiki wanazungumza kuhusu mambo mengi. Lakini kuomba kwa mahitaji ni sehemu muhimu ya sala. Unaweza kusema 'Mungu anajua mahitaji yetu. Kwa nini tunahitaji kuomba?' Mimi najua mahitaji ya watoto wangu, lakini naturahi wanaponiomba. Mungu anafurahi tunapoonyesha kwamba tunamtegemea, na tupo tayari kumweleza mahitaji yetu. Na tunapoomba na tunaona majibu, inaimarisha uhusiano wetu.

Pili, kusali kuna thawabu kwake. 'Usali mbele za Baba yako aliye sirini;

na Baba yako aonaye sirini atakujazi' (Mat 6:6) Tunapewa nguvu mpya. Tunajazwa imani na kuzimwa kiu. Tunapewa uhakika kwamba sisi tu wana wake Mungu.

Tatu, kuomba kuna nguvu hata kubadilisha mambo yalivyo. Hatujui kabisa jinsi Mungu anavyotenda hivi, lakini mara nyigi tumeona kwamba mambo yaliyoonekana kama hayawezekani yanafanikiwa tunapoomba. Mwenyezi Mungu anatualika kufanya kazi pamoja naye, na anasubiri mpaka tuwe tayari kufanya kazi hii.

## **Je, Mungu anajibu sala kila tunapoomba?**

Tukitazama Injili ya Mathayo sura ya 7, mstari wa 7, tunasoma 'Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni nanyi mtafunguliwa' Lakini, inaonekana kwamba mara nyigi, hatuoni matokeo ya sala zetu. Je ahadi hii ni bure? La, hasha! ila kuna sababu nzuri kwa nini hatupati kila tunachokionba.

Yawezekana tunaishi katika hali ya kutomtii Mungu. Tukiwa na mioyo migumu, na tunajua kwamba tunakosa, lakini hatutaki kubadilisha, basi urafiki wetu na Mungu unavunjika, na hatuwezi kutazamia kwamba atatusikiliza. Tukimkataa Mungu, hatuwezi kutazamia kwamba atajibu sala zetu.

Wakati mwengine, hatuombi kwa madhumuni mazuri. Yakobo aliandika 'Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu' (Yakobo 4:3)

Tukiomba mali kwa sababu ya uchoyo wetu, au kwa msaada kwa ajili ya rafiki ili asitusumbue, tunaomba vibaya. Nia yetu iwe kwanza kwa kazi ya Mungu, na baadaye tu kwa mahitaji na matakwa yetu. Tutaona kwamba kadiri tunavyomfahamu Mungu ndivyo tutakavyopata tunavyoviomba, kwa sababu nia zetu zitaanza kufanana na nia yake Mungu.

Labda tunaomba vitu vibaya. Mtoto akiomba kisu kikali, Baba mzuri atamkataza kwa sababu anajua kwamba anaweza kujiumiza. Mungu atatukataza tukiomba vitu ambavyo vitatumiza, au vitaumiza wengine, sasa au baadaye. Au labda atasema 'subiri'. Lakini tunajua kwamba Mungu ni Baba mzuri; akikataa, tuamini kwamba anajua vizuri kuliko sisi tulivyotaka.

## Tuombeje?

Hakuna sheria kuhusu jinsi ya kusali kwa sababu ni urafiki. Lakini watu wengi wanasaidiwa kwa kuwa na mfano wa sala ili wakue katika urafiki huo. Mfano mmojawapo ni huu.

1. Kumsujudu Mungu Tuanze kwa kukumbuka jinsi Mungu alivyo, na matendo yake anayoyafanya kwetu na ulimwenguni kote.
2. Kukiri dhambi zetu tukiomba msamaha wake
3. Kumshukuru kwa afya, marafiki, jamaa na vitu vingine
4. Kuomba mahitaji kwa ajili yetu na wengine

Mfano mwengine ni kufuata maneno ya sala ya Bwana (Mat 6:9 - 13)

*Baba yetu uliye mbinguni:* Tumshukuru Mungu kwa jinsi alivyo, na kwa matendo yake anayoyafanya kwetu na ulimwengu wote. Tunamshukuru kwa majibu yake ya sala zetu.

*Jina lako litukuzwe:* Jina la mtu katika lugha ya Kiebrania linaonyesha tabia ya mtu. Kuomba kwamba jina lake litukuzwe ni kuomba kwamba watu wamheshimu; na sisi wenyewe, na makanisa yetu na jamii yetu.

*Ufalme wako uje:* Ufalme wa Mungu ni utawala wake. Utakamilishwa Yesu atakaporudi tena. Lakini umeanza kuingia duniani Yesu alipokuja mara ya kwanza - alionyesha dalili yake kwa miujiza yake. Tunapoomba 'Ufalme wako uje' tunaomba kwamba Mungu atatawala sasa hivi na hata siku za mwisho. Tunaomba arudi tena hivi karibuni. Lakini pia tunaomba kwamba sasa hivi watu waponywe, waokoke, wajazwe Roho mtakatifu ili wamtumikie Mungu pamoja na kuonyesha ufalme wake hapa duniani.

*Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni:* Tunampa Mungu mizigo yetu, na tunamwamini kutuongoza.

*Utupe leo riziki yetu:* Tunaomba kuhusu mahitaji yetu ya kila siku - kazi zetu, watoto wetu, mambo yanayotuhangaisha n.k.



*Utusamehe makosa yetu kama tunavyosamehe waliotukosea:* Ni kweli kwamba tunapoamini Mungu mara ya kwanza tunasamehewa dhambi zetu zote. Lakini, tunapoishi maisha ya kila siku, tunaendelea kukosa. Ni kama kwamba tunapokuja msalabani mara ya kwanza, tunaogeshwa kabisa. Lakini tunapotembea duniani, miguu yetu inachafuka, na tunahitaji kunawishwa tena. Nafasi yetu mbinguni inahakikishwa mara ya kwanza, lakini urafiki na Mungu unavyoendelea kuhtarishwa, ndivyo na furaha inaharibika.

Tunapoelewa kweli kadiri tunavyosamehewa, itatufanya tuweze kuwasamehe waliotukosea pia. Hatutaweza kukataa.

*Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu:* Mara nyingi tunajua mambo yanayotupa shida sisi binafsi. Tunaomba msaada wa Mungu kwa kukwepa mambo hayo, na kumfuata vizuri

## **Tuombe Lini**

Agano Jipya linatuhimiza kusali wakati wote. Hatuhitaji kuwapo mahali maalum, tunaweza kusali katika basi, tunapotembea, tunapoosha vyombo, tunapokaa kitandani, wakati wowote. Lakini, kama katika ndoa, ni vizuri pia kuwa na wakati maalum unaowekwa hasa kwa ajili ya kuzungumza. Yesu mwenyewe alienda mahali pasipokuwa na watu ili kusali. Mara nyingi, wakati tunaposoma Biblia ni wakati mzuri kusali pia, hata kwa dakika chache kila siku. Ni vizuri kuwa na utaratibu; la sivo tutakuta kwamba mara nyingi siku imekwisha na hatujatengeneza nafasi.

Ni vizuri pia kukutana na wenzetu kwa ajili ya kusali - kufanya hivi kunatujengea imani yetu pamoja na kututia moyo, na Mungu yupo kwa njia maalum. Ingawa tunaweza kuogopa sana wenzetu, baadaye tutazoea, na tutakuta kwamba tunapata nguvu mpya tunapofanya hivi.

Kusali kuna nguvu sana. Tunaposali, Shetani anatetemeka kwa hofu kwa sababu anajua kwamba nguvu ya Mungu inaweza kuingia katika maisha yetu. Lakini, kwa msaada wa Mungu, tunaweza kushinda na kukua katika maisha yetu ya sala, na tutaona baraka nyingi katika maisha yetu.

## **Maswali**

1. Umeona majibu ya sala? Nini? Lini?
  
  
  
  
  
  
2. Kwa nini tusali?
  
  
  
  
  
  
3. Kwa nini hatupokei kila tunachokiomba?
  
  
  
  
  
  
4. Je, kweli Mungu anabadilisha tukio tunapoomba?
  
  
  
  
  
  
5. Mambo gani ni muhimu kuingiza katika sala zetu wakati wa kusali?
  
  
  
  
  
  
6. Unafikiri ni vigumu kusali kwa sauti mbele ya watu wengine? Kwa nini tufanye hivyo?

# Roho Mtakatifu ni nani?

Kwenye Ibada yote tunamtaja Roho Mtakatifu, lakini, Wakristo wengi hawajui sana kuhusu yeye. Ni mtu anayetajwa tu. Katika historia, kanisa limemwacha upande, hawajamwelewa sana. Kwenye sura hii tutatazama kazi yake na nafsi yake.

## Roho Mtakatifu katika Agano la Kale

1. Roho Mtakatifu alikuwepo, wakati Mungu alipoumba ulimwengu. Anatajiwa katika mistari ya kwanza ya Biblia. Alileta taratibu kutoka kwa kisicho na taratibu. (Mwa 1:2) Alimpa maisha binadamu. (Mwa 2:7) Neno kwa ‘pumzi’ lina maana ya ‘roho’ pia - yaani, analeta maisha kwa wale ambaeo waliumbwaa kutoka mavumbi. Na hata leo, analeta taratibu katika maisha yetu ya ovyoovyo, na analeta maisha sehemu zile zenye watu wale waliopo katika kifo
2. Aliwatokea baadhi ya watu, kwa wakati fulani na kwa kazi maalum.

Bezalel	Kwa kazi ya kupamba hekalu	(Kut 31:1 - 5)
Gideon	Kwa kuongoza watu wa Mungu	(Waamuzi 6:14 - 16,34)
Samson	Kwa nguvu	(Waamuzi 15:14 - 15)
Isaiah	Kwa unabii	(Is 61:1 - 3)

Lakini, baadaye, Roho Mtakatifu aliwaacha tena, kazi ilipokuwa imekwisha

3. Katika Agano la kale, Mungu alitengeneza makubaliano na watu wake. Mradi walizitii amri zake na kumfuata, atakuwa Mungu wao kwa njia ya karibu zaidi kuliko mataifa mengine. Lakini, watu walishindwa kutii. Hawakuweza. Kwa hiyo Mungu aliahidi kitu kipyaa. Alisema kwamba atatengeneza makubaliano mapya. Badala ya kuandika amri katika vipande vya mawe, ataziandika mioyoni mwa watu, ili waweze kuzijua na kuzifuata. Aliahidi kwamba, baadaye, si makuhani tu ambaeo watamfahamu Mungu, lakini itawezekana kwa watu wote, watu wa kawaida pia. Wote wataweza kumfahamu Mungu na kuwa rafiki naye.

- Yeremiah 31:31 - 34
- Ezek 36:26 - 27
- Ezek 47
- Yoeli 2: 28 - 29

Lakini ahadi haikutokea kwa miaka 300. Watu walianza kusahau.

## **Roho Mtakatifu katika Agano Jipyä**

1. Yesu alipokuja, Roho wa Mungu aliwatokea baadhi ya watu tena kama siku zilizopita.

Yohana Mbatizaji (Lk 1:14 - 15)

Mariamu (Lk 1:35)

Elizabeti (Lk 1:41)

Zakaria (Lk 1:67)

Simeoni (Lk 2:25 - 27)

Aliwatokea watu wachache kwa kuwawezesha kwa kazi fulani maalum, kama alivyofanya mwanzoni

2. Yohana Mbatizaji alitangaza kwamba Yesu ataleta uwezo kwa wote kujazwa na Roho Mtakatifu. (Lk 3:16)
3. Yesu alijazwa hasa na Roho Mtakatifu kwa kazi yake. (Lk 3:22, Lk 4:1, Lk 4:14, 21)
4. Yesu alisema kwamba atawajaza watu wote na Roho Mtakatifu. (Yoh 7: 37 - 39, Lk 24:49, Mdo 1:4,5,8)
5. Wakati wa Pentekoste, wanafunzi wa Yesu walikuwa wa kwanza kujazwa na Roho Mtakatifu, kama mwanzo wa kipindi kipyä. Kuanzia wakati ule, Roho Mtakatifu anapatikana akiishi ndani yao wote walio wa Yesu. (Mdo 2:2 - 4, 33, 39)

## **Kazi za Roho Mtakatifu**

Yesu alisema kwamba kuwa Mkristo ni kama kuzaliwa tena (Yoh 3:5 - 8) Kuzaliwa mwilini haitoshi. Tunapoanza kuwa wakristo, tunazaliwa tena rohoni. Labda hatuwezi kusema ilitokea lini - kama kuzaliwa kwetu, labda hatujui tarehe yake. Hivyo tunajua moyoni kama tunaishi katika mambo ya Mungu, au kama tunahudhuria kanisani tu bila kuguswa.

Hatzaliwi peke yetu. Tunazaliwa katika familia. Tunapozaliwa Rohoni, tunazaliwa katika familia ya Wakristo. Kazi za Roho ni katika familia hii. Kwa mfano, anatutumainisha kwamba sisi ni watoto wa Mungu, na anatusaidia kukua na kufanana naye. Anatuunganisha na dada na kaka zetu katika Kristo, na kutusaidia kuleta watu wengine katika familia ya Kristo. Mpaka watakapoanza kuwa wakristo, kazi ya Roho Mtakatifu ni kuuhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu (Yoh 16: 7 - 15)

## **1. Watoto wa Mungu**

Kazi ya Roho Mtakatifu ni kutufanya kujua kwamba sisi tu wana wa Mungu (Rum 8 14ff).

Katika jamii ya Warumi, kwa mtu kuwa na warithi, ama alichagua watoto wake, au aliweza kumchagua mwingine kuwa kama mwana. Ni kama hivi kwetu. Mungu ametuchukua na kutufanya kuwa wana na warithi wake. Tulikuwa kama yatima, lakini ametupa nafasi katika familia yake, na sasa sisi ni wana wa Mungu. Hakuna nafasi kulinganisha na hii, kwamba sisi ni wana wa Mfalme, wana wa Mungu mwenyezi mwenyewe.

Pili, anatupa ujasiri kuwa na urafiki na Mungu kama watoto wake. Ni kama watoto wa rais hawatamwita ‘Mheshimiwa Rais’. Watamwita ‘Baba’. Na sisi tunaweza kumfahamu Mungu si kama Mwenyezi tu, lakini pia kama Baba yetu. Na kazi ya Roho Mtakatifu ni kutufanya kujua miyoni kwamba ni hivyo, kwamba sisi ni watoto wapendwa wa Mungu. Ni kama kuwa mtoto badala ya mtumwa. Tunajijua kama watoto wapendwa wa Mungu.

Tatu, tunajua kwamba mwishoni, tutakuwa warithi wa Mungu. Bila shaka mwana anarithi vitu vya baba yake atakapokufa. Na kwetu sisi, Mungu ameweka furaha ya milele mbinguni tutakapokufa. Tunaweza kuwa na hakika kwamba sisi ni watoto wa Mungu.

## **2. Urafiki wetu kukua**

Tunapozaliwa, si mwisho, ni mwanzo tu wa urafiki wetu na wazazi wetu. Vivyo hivyo, tunapoanza kuwa wakristo, si mwisho, lakini mwanzo wa maisha mapya. Roho Mtakatifu yupo kutusaidia kukua katika Kristo.

Efe 2:18

Anatusaidia kusali (Rum 8: 26)

Anatusaidia kusoma Biblia (Efe 1:17 - 18)

## **3. Kufanana na Mungu**

Mara nydingi tunaona kwamba watoto wanafanana sana na baba au Mama yao. Na sisi tunaitwa kufanana na Mungu. Roho Mtakatifu anaotesha ndani yetu matunda yake ambayo yanatupa tabia kama Mungu alioionyesha katika Yesu. (Gal 5:22, 2 Kor 3:18, 2 Kor 2:14)

## **4. Umoja katika familia**

Mungu anataka, kama mzazi yejote, kwamba mtakuwa na umoja ndani ya familia - kwamba kaka amtuze kaka na dada ampende dada. (Efe 4: 4 - 6) Roho Mtakatifu anaweza kutusaidia kuishi pamoja kwa amani na upendo ingawa sisi ni watu tofauti, kutoka kabilia tofauti na nchi mbalimbali, na wenye maoni mbalimbali.

## **5. Vipawa katika familia**

Ingawa watu wa familia wanafanana, pia, ni tofauti. Hata mapacha hutofautiana. Vivyo hivyo, katika kanisa, tupo tofauti, na uwezo tofauti na vipawa tofauti. Kwa hiyo kila mtu ana kitu tofauti cha kuleta kwa faida ya kanisa. 1 Kor 12:7 - 11. Lakini, tunahitaji wote kutumia vipawa vyetu. Katika kanisa la leo, kuna tatizo kubwa la kutoajiri. Viongozi na wengine wachache wanafanya kazi zote, na wengine wanahuduria tu, kuangalia kazi yao. Ni kama mashindano ya mpira - watu wengi wavivu wanaangalia watu 22 wanaocheza na wao wanapumzika tu! Vipawa vyetu tumepokea kila mtu bila kuhitaji kulipa, kwa faida ya kanisa zima. Tunahitaji kuvitumia. Wachungaji hawapo kufanya ukasisi wao, wapo ili kusaidia kila Mkristo afanye ukasisi wake.



## **6. Kuongeza familia**

Kazi ya mwisho muhimu ya Roho Mtakatifu ni kutupa nguvu ili kuwaleta wengine. Lengo la kanisa si tu kujisikia vizuri kama familia. Ni kuleta wengine walio nje ya familia, ili wajue habari njema na kuongezwa katika familia ya Kanisa. Tokeo moja la kazi ya Roho Mtakatifu ni kwamba tunataka kuwaambia wengine kuhusu imani yetu, na tuna nguvu kuwaambia pia. (Mdo 1:8)

Kila Mkristo amepewa Roho Mtakatifu alipoanza kuwa mkristo. Ni alama ya kuwa mkristo. (Rum 8:9) Lakini, tunaitwa kujazwa kabisa Roho Mtakatifu. (Efe 5:18) Tunahitaji kuomba, kuendelea kutafuta nguvu ya Mungu katika maisha yetu. (Lk 11:13) Ni ombi ambalo Mungu anafurahi sana kusikia na kujibu.

## **Ninawezaje kujazwa Roho Mtakatifu?**

Kama wakristo, sisi sote tuna Roho Mtakatifu akikaa ndani yetu.

Lakini kutakuwa na nyakati maalum tunaposikia kwamba yumo ndani yetu kwa njia maalumu. Ni kama baba anapotembea barabarani na mtoto wake. Labda mara moja atasimama na kumkumbatia mtoto wake, na kumbeba kwa muda mfupi, kwa sababu anampenda sana. Hivyo, tutakuwa na wakati fulani tunaposikia kwamba tupo karibu zaidi na Mungu Baba yetu. Tunajazwa kabisa na Roho Mtakatifu.

## **Kuna matokeo gani?**

Kwanza tunajisikia uwepo wa Mungu ndani yetu kwa nguvu. Si jambo tunalolielewa kwa kichwa tu - upendo wa Mungu unafika moyoni kabisa.

Pili, hatuwezi kuacha kumsifu Mungu. Tunashangaa upendo wa Mungu mpaka hatuwezi kukaa kimya - itabidii tumshangilia Mungu na kuwaambia wengine kuhusu ajabu hii.

Tatu, wengine wanapewa uwezo kusema kwa lugha nyingine, inayowasadida kusali, kwa ajili yao wenyewe na kuwaombea wengine, na kumwabudu Mungu. Inawasadida kusali nyakati ambazo wameishiwa maneno yanayofaa, au hawajui waombe nini. Hii ni baraka kutoka kwa Mungu, lakini haina maana kwamba wale wanaosema hivyo ni Wakristo wa hali au kiwango cha juu kuliko wenzao, au wanamfahamu Mungu zaidi. Tena, kanisani, Paulo alisema ‘afadhali kusema maneno matano yanaoeleweka kuliko maneno kumi elfu katika lugha nyingine’ (1 Kor 14:19)

Tukitaka kujazwa tena na Roho Mtakatifu, tumwombe Mungu. Lakini tusitafute kujazwa ili tujisikie vizuri, bali kutuandaa kumtumikia Yesu kwa upya. Tunaweza kusali peke yetu, lakini afadhali kusali pamoja na rafiki ambaye ni Mkristo.

1. Uombe Mungu akusamehe dhambi zako zote.
2. Utubu yote ambayo unajua ni mabaya katika maisha yako.
3. Uombe kujazwa Roho Mtakatifu
4. Ukitaka, ufungue mdomo na kuanza kusema maneno yanayoingia mdmoni ya kumsifu Mungu, hata ingawa ni maneno ambayo huyaelewi mwenyewe. Mungu ataelewa!

Luka 11.11 - 13 ‘Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe? au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? au akimwomba yai, atampa nge? Basi ikiwa ninyi mlío waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?’ Tusiogope, wala kujisikia kwamba hatustahili wala hatutapewa. Mungu ameahidi, na atafanya.

Paulo anaposema tujazwe na Roho Mtakatifu (Efe 5:18), anatumia neno la Kigiriki lenye maana kwamba tuendelee kila wakati kujazwa Roho Mtakatifu. Biblia inasema kwamba Petro alijazwa na Roho Mtakatifu mara tatu hata katika sura ya 2 hadi ya 4 ya Matendo ya Mitume. Haitokei mara moja tu, lakini ni kitu ambacho kinaendelea na kukua katika maisha yetu, ili tukue katika kumtumikia Mungu.



## **Maswali**

1. Kuna tofauti gani kati ya kazi ya Roho Mtakatifu katika Agano la Kale na Agano Jipya?
2. Roho Mtakatifu anafanya kazi gani katika maisha ya mtu kabla hajawa Mkristo?
3. Anatusaidiaje kukua katika imani yetu, baada ya kuokoka?
4. Roho Mtakatifu anawezeshaje kanisa kukua na kuongezeka?
5. Nini kinatuzuia kujazwa Roho Mtakatifu kila wakati?

## **Nawezaje kushinda uovu?**

Tangu zamani, watu wamemwamini Mungu aliyeumba vyote vilivyo vizuri. Na tangu zamani pia, watu wameamini mtu anayesababisha vyote vibaya - wanamwita Shetani, au Ibilisi Kwenye Biblia, hatuambiwi kuhusu mwanzo wake, ila kwamba ni nafsi, anayeongoza mapepo yake. Tazama Efe 6:11 - 12

Ni mjanja, anafanya hila (v11), mwenye nguvu (v11), mbaya (v12). Kwa hiyo tusishangae anapotushambulia

## **Kwa nini tukiri kwamba yupo?**

Kwanza, kwenye Biblia, tunajifunza kuhusu Shetani. Yesu alimjua Shetani, na hivyo kazi yake ni kuwaokoa watu kutoka katika nguvu za Shetani maishani mwao. Katika Waraka anatajwa mara nyingi (k.m. 1 Pet 5:8 - 11, Efe 6:1 - 12)

Pili, tunaweza kuona kazi yake ulimwenguni, sasa na muda uliopita. Kuna majeshi mabaya katika kila kipindi cha historia, kipinga kazi ya Mungu inayoendelea.

Kuna makosa mawili kuhusu Shetani. Kwanza ni kumhesabu kama mtu asiyе na nguvu. Hilo linamwezesha kufanya kazi yake vizuri zaidi akijua kwamba watu wana mashaka kuhusu kuwako kwake, au wanamsahau.

Pili ni kumjali mno na kazi yake. Hairuhusiwi kucheza na mambo ya giza (Kum. 18:10, Law 19:20ff, Gal 5:19ff, Ufu 21:8, 22:15). Ikiwa tumefanya hivi, tutubu na kuomba msamaha kwa Mungu. Hata wakristo wengine wanahubiri sana kuhusu Shetani, na maana ya maandishi mbalimbali kwa mfano katika Ufunuo au Danieli. Ingawa ni muhimu kujua kuhusu mambo haya, kiini cha mawazo yetu kiwe juu ya Mungu na mwana wake Yesu Kristo.

## **Shetani anatumia mbinu gani?**

Lengo la Shetani ni kudhuru kila binadamu. Anataka tufuate njia ya kufikia uharibifu. (Yoh 10:10) Kwa hiyo, lengo lake la kwanza ni kuzuia watu wasije kwake Kristo. 2 Kor 4:4

Tunapofuata njia ya uharibifu, Shetani hatusumbui. Mara tunapoolekea njia ya kutufikisha uzima wa milele, Shetani hafurahi na atajitahidi kutugeuza.

Kazi yake ya kwanza ni kuleta mashaka. Alianza hivyo kwenye bustani ya Edeni ‘Je, *Kweli* Mungu alisema....’ Tena kwenye mateso ya Yesu ‘Kama wewe ni Mwana wa Mungu...’ Baada ya kuleta mashaka, anaweza kuingiza kishawishi kwa urahisi zaidi. ‘Je, *kweli* Mungu alisema kwamba usifanye

hivyo....?' au 'Ikiwa wewe kweli ni mkristo....' Ikiwa anaweza kuharibu uhakika wetu kwa Mungu, ameshinda nusu ya vita vyake.



Tutatazama kwa karibu zaidi mbinu za Shetani bustanini. Mwanzo 2:16 - 17. Mungu alitoa ruhusa kwa Adamu na Hawa kuchukua matunda yoyote bustani ila moja. Shetani aliwakumbusha kuhusu kile kitu kidogo ambacho hawakuruhusiwa kufanya, na kukisababisha kuonekana kama kitu kikubwa (Mwa 3:1) Hajabadili. Bado, anaacha vitu vyote ambavyo tumepewa na Mungu (1 Tim 6:17) Anaacha faida yetu inayotokana na kutembea na Mungu, kuwa sehemu ya familia yake, faida ya ushirikiano na wenzetu, ya starehe ya ndoa ya kikristo, na msaada wa Mungu katika maisha yetu. Anaacha vitu vyote vizuri Mungu alivyotupa - furaha yote ya kuishi hapa ulimwenguni. Badala yake anatukumbusha kuhusu vitu vichache ambavyo haturuhusiwi kufanya - hatuwezi kulewa, kukutana kimwili nje ya ndoa. Hivi ni vitu vichache tena vyenye sababu kubwa kwa nini tusivifanye.

Mwishoni, anakataa adhabu. (Mwa 3:4) Anasema haidhuru kutomtii Mungu. Anatuambia kwamba Mungu hataki vitu vizuri kwetu, tutakosa vitu vizuri tukimfuata. Kwa kweli tunajua kwamba ni kinyume chake. Tukiasi, itatusababisha kukosa furaha ambayo Mungu ametuvekea. Kwa mfano;

Kwanza Adamu na Hawa waliona aibu. (mst 7). Hawakutaka wengine wawaone. Sisi sote tunasikia aibu kuhusu makosa yetu. Karibu kila mtu ana kitu kwenye maisha yake ambacho asingependa mwenzake kujua.

Pili, urafiki wao na Mungu ulivunjika. (mst 8) Walijificha. Na sisi tunaweza kukwepa mambo ya Mungu tukijua kwamba tumekosa. Tunataka kujificha. (Unaweza kuona kwamba mara moja, Mungu alianza kujaribu kumvuta Adamu tena (mst 9))

Tatu, walibishana wao kwa wao. Adamu alimlaumu Hawa, Hawa alimlaumu Shetani. Tukikosa, tutaanza pia kubishana na wenzetu - ndoa inavunjika, familia zinakataa wenzao, mataifa yanapigana vita.

Nne, mwishoni, walipewa adhabu ya Mungu. (mst 14ff) Kweli wamejiletea shida. Na sisi tukikosa tutabeba matokeo ya makosa yetu. Kwa mfano, Daudi alipozaa nje ya ndoa, alitubu, alisamehewa lakini bado mtoto alikufa (2 Sam 11 - 12)

Tumeona kwamba Shetani ni mdanganyifu. Pia ni mshtaki. Maana ya 'Shetani' katika Kiebrania ni mshtaki. Anamlaumu Mungu mbele ya watu. Anamshtaki Mungu kwa kila kitu. Anasema Mungu si mwaminifu. Pili, anashtaki wakristo mbele ya Mungu. Anatusababisha kujisikia tuko hatiani.

Kujaribiwa si sawasawa na kukosa. Wakati fulani Shetani anaweka mawazo fulani kichwani mwetu kufanya kitu ambacho tunajua ni kosa. Wakati huu huu tunahitaji kukata shauri kufuata, au kutupilia mbali. Tukicheza nayo, tunaanza kukosa. Tukiyatupa mbali, tunafanya kama Yesu (Ebr 4:15) Lakini mara nydingi kabla hatujapata nafasi ya kuyatupa, Shetani anasema 'Wewe, unajiita mkristo. Unafikiri mawazo mabaya! Huwezi kuwa mkristo! Umekosa sana.' Anataka tukubali, na kusema 'kweli, nimeanza kukosa. Nimeshashindwa, Si muhimu sasa nikiendelea kukosa,' Na tunaendelea na makosa, na tunajiletea aibu na hatia. Shetani anataka tuwe na kawaida mbaya. Tukikosa mara ya kwanza tunajisikia vibaya. Mara ya kumi, tunaacha kujisikia vibaya kabisa. Tunakuwa tumeshakamatwa na dhambi. Tupo kwenye njia ya kufika upotovuni.

## **Cheo chetu ni kipi?**

Katika Wakolosai 1:13, tunakumbushwa kwamba Mungu 'alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa mwana wa pendo lake' Tulikuwapo katika nguvu za giza - yaani utumwa wa dhambi, mauti, uharibifu. Lakini ametuleta katika ufalme wa nuru, yaani msamaha, uhai, wokovu. Ni kama kuajiriwa upya. Mtu aliyejaujiri zamani akija na kusema 'kwa nini hupo kazini kwangu?' Itakubidii umwambie 'nimemaliza mkataba wangu nawe, na sasa nina kazi nydingine. Sihitaji kufanya kazi yako tena' Ni hivyo na sisi. Sasa tupo katika ufalme wa Mungu. Shetani akija kutujaribu, tumwambie 'mimi ni mkristo sasa. Deni langu limelipwa. Sihitaji kukutii tena'

Shetani ameshindwa msalabani. Yesu 'akiisha kuzivua enzi na

mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo' (Kol 2:15) Sasa tunaishi katika kipindi cha mwisho wa vita. Adui yetu bado ana uwezo wa kutuumiza, kama adui wa vita anayekimbia bado anaweza kuwaa wanajeshi wachache njiani. Mwisho wake unahakika, hata ingawa tunapokuwepo sasa hivi, njia inaonekana bado ndefu.

## **Je, Tutajilindaje?**

Paulo anatushauri 'Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzishinda nguvu za Shetani' (Efe 6:11) Tunahitaji silaha zote - haifai kuvala nusu tu! Anataja sehemu sita.

### **1. Vaeni Kweli viunoni**

Tunahitaji kuelewa misingi ya Imani yetu, kuingiza mafundisho ya kikristo kichwani ili tuwe tayari kukataa uongo wa Shetani. Tusome Biblia siku kwa siku, tusikilize mahubiri kanisani, tusome vitabu vya kikristo, tusikilize maneno ya Biblia katika nyimbo. Tukifanya hivyo, tutajifunza kutambua ukweli ni nini, na kutosikiliza sauti ya uwongo.

### **2. Diri ya Haki kifuani**

Haki yetu inatokana na kazi ya Yesu msalabani. Inatuwezesha kuwa na urafiki na Mungu, na kuishi maisha ya haki. Yakobo alisema 'Mpingeni Shetani naye atawakimbia. Mkaribieni Mungu naye atawakaribia nyinyi.' (Yak 4:7 - 8) Tukianguka, tusimame tena kwa haraka. Tumwambie Mungu kwamba tumekosa, na kuomba kusamehewa. Basi tutasimama tena kwa haki mbele ya Mungu



### **3. Kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani**

Tuwe tayari kumshuduhia Kristo. Ni vigumu kukaa tu bila shuguli na kuwa wema. Ikiwa tunatumia nguvu zetu kwa kufanya kazi ya Mungu, hatutakuwa na nafasi au nguvu ya kutii sauti ya Shetani. Na tukisema kwamba sisi ni wakristo, tutaangaliwa na familia na marafiki, kuona kama ni kweli au sivyo - hii itatusaidia kujilinda

## **4. Ngao ya Imani**

Imani ni kushika ahadi ya Mungu na kuiamini. Shetani atatupa mishale ya mashaka, lakini tusimame imara, kwa sababu tunamfahamu Mungu wetu na uaminifu wake

## **5. Chapeo ya Wokovu**

Wokovu wetu ni wa zamani, wa sasa na wa baadaye. Ni wa zamani kwa sababu tumeshaokolewa na adhabu ya dhambi. Imekwishatokea kwa sababu ya msalaba. Tunahitaji kuamini tu. Ni wa sasa kwa sababu tunaokolewa na nguvu ya dhambi. Kidogo kidogo tunajifunza kusimama imara na kukataa kumtii Shetani anapotujaribu. Ni wa baadaye kwa sababu siku ya mwisho, dhambi itakwenda, na tutakaa mbinguni na Mungu daima. Tunahitaji kushika kweli hizo kichwani, tusimame imara

## **6. Upanga wa Roho**

Upanga wa Roho ni neno la Mungu. Alipojaribiwa, Yesu alijibu kwa kutumia neno la Mungu. Tujifunze mistari kutoka Biblia ili tujue kumjibu Shetani anapotusumbua, na tujikumbushe ahadi za Mungu. Hii ni silaha pekee ya kupambana. Ni muhimu kabisa tuisome na kujifunza.

## **Tutashambulia au kupambana vipi?**

Kwanza tunaitwa kuomba. ‘Silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome’ (2 Kor 10:4) Maombi yalikuwa muhimu sana maishani mwa Yesu, na iwe hivyo kwetu pia.

Pili, matendo yetu. Maombi na matendo yanakwenda pamoja. Tuhubiri Injili, na kuionyesha katika maisha yetu. Tukiishi vizuri, adui zetu hawataweza kutulaumu.

Biblia haisemi kwamba kuna nguvu mbili zilizo sawasawa, Shetani na Mungu. Bali, inasema kwamba Mungu ni mwenyezi, na Shetani ameshindwa. Ni kweli, anatusumbua sasa, lakini mwisho wake una hakika. Kwa hiyo, tusiogope usumbufu wa Shetani, bali kutazama ushindi wa Mungu wetu, na kumtazama Yesu kuliko mambo yote, na pole pole tutashinda.

## Maswali

1. Shetani anatumia mbinu gani katika maisha yetu? Umeona hii?
  2. Kuna tofauti gani kati ya kujaribiwa na kutenda dhambi yenyewe? Kwa nini hii ni muhimu?
  3. Tunapokubali kuwa wakristo, cheo chetu mbele ya Shetani kinabadilishwaje? Ina matokeo gani katika maisha yetu?
  4. Katika Waefeso sura ya 6, Paulo anataja silaha sita. Kila silaha ina maana gani kwako?

# Mungu anatuongozaje?

Sisi sote tunahitaji kuamua kuhusu mambo fulani. Tunaamua kuhusu kazi zetu, fedha zetu, watoto wetu, kufunga ndoa, kujenga nyumba, matumizi ya muda wetu n.k. Mara nydingi ni maamuzi muhimu. Tunahitaji msaada wa Mungu.

Kuongozwa kunatokana na uhusiano wetu na Mungu. Anaahidi kwaongoza wale wanaotembea naye. (Jn 10:3 - 4) Anataka tujue njia zake. Anatupenda na kutaka kuzungumza nasi kuhusu maisha yetu - mambo madogo na makubwa.

Mungu anasema kwamba ana mipango na makusudi katika maisha yetu. Wengine hawataki iwe hivyo. Wanasema 'sifikiri nataka kufuata mpango wa Mungu kwa maisha yangu. Sijui kama nitaupenda' Lakini tusiwe na hofu. Mtume Paulo anasema kwamba njia ya Mungu kwetu ni njema na ni ya ukamilifu (Rum 12:2) (Tazama pia Yer 29:11) Mara nydingi tunazungukwa na watu ambao wameharibu maisha yao kwa sababu hawajafuata nia ya Mungu na mipango yake.

Kama tunataka kufuata mipango ya Mungu, tunahitaji kumwombia. Mungu ametuonya kuhusu kufuata njia zetu bila kuzungumza naye kwanza. Au Mara nydingi, tunafanya mpango, halafu baadaye tunaomba Mungu aubariki.

Mungu anatuongoza tunapokuwa tayari kumfuata badala ya kufuata njia zetu. Tuwe na moyo kama wa Mariamu (Lk 1:38) Tukiwa tayari kumfuata, yupo tayari kutuonyesha njia yake. (Zab 37:5)

Lakini tutajuaje kwamba huu ni uongozi wa Mungu? Kuna njia mbalimbali anaweza kutumia. Ikiwa ni jambo muhimu, anaweza kutumia njia zaidi kuliko moja pamoja kutuonyesha.

## **Katika Biblia**

Katika Biblia, Mungu ameandika nia yake kwa watu wote kwa jinsi wanavyoishi pamoja, na ameandika uongozi wake kwa maisha ya kila siku pale. Kwa mfano, mtu anaweza kusema 'hampenda sana Mama huyu, naona kwamba Mungu ameniongoza kuishi naye nyumbani.' Lakini, ikiwa ameshaoleta na mwagine, Mungu ameshatuonyesha nia yake. Amesema 'Usizini' (Kut 20:14) Unaweza kuwa na hakika kwamba Mungu hasemi kwamba tumchukue mke wa mwagine.

Tena, tunaweza kusema 'sitalipa kodi yangu ili niwe na fedha ya kutosha kwa nguo, au hata kwa sadaka ya kanisa' Mungu ameshasema kwamba tulipe kodi yetu, (Rum 13:7) kwa hiyo, hatuhitaji kuomba uongozi wake zaidi.

Tukisoma Biblia, tutajua. Na tusipofuata njia yake ambaye tumeshajua, tunatazamiaje kwamba atatuongoza katika maamuzi maalumu?


Tumeona kwamba Biblia inasema ‘mambo ya msingi’ ambayo tunaweza kufuata, lakini haisemi kuhusu kila jambo. Kwa mfano, tunajua kwamba ni kawaida kwa watu kuoa, ingawa wachache wanaitwa kuishi peke yao. (1 Kor 7:2) Tunajua kwamba afadhali kwamba wakristo waoane na wakristo wengine (2 Kor 6:14) Tunajua kwamba ndoa ni ya maisha yote. Lakini haisemi ‘Yohana, umwoe Mariamu’ au ‘Umwoe Rehema’

Lakini, tunaposoma Biblia, tunaweza kukuta kwamba maneno yake yanahusu maisha yetu hasa wakati wa sasa. Mungu anaweza kuchukua maneno yake na kuyatumia kutuonyesha jambo fulani tunalolihitaji kujua. Lakini, hatuwezi kuchukua maneno yoyote bila kuyatazama kuona ‘je maana yake kwa wakristo wa kwanza ni nini?’, na hatuwezi kuchukua maneno machache bila ya kutazama sura nzima kuona maana yake kweli. Lazima tushike maneno ya Biblia kwa ujumla kwanza, halafu kutazama mistari tunayoisoma kuona kama kweli inakubaliana na mafundisho ya Biblia, au imeandikwa kuonyesha mfano mbaya au kutuonya. Afadhali tukipata kawaida ya kusoma sehemu ndogo kila siku, halafu Mungu anaweza kutumia maneno haya kutuongoza wakati tunapohitaji msaada.

## **Roho wa Mungu**

Tunapoanza kuwa wakristo, Roho wa Mungu anakuja kuishi ndani yetu. Anaanza kusema nasi. Tunahitaji kuanza kutambua sauti yake. Tunatambua sauti ya mama zetu mara moja. Kama ni rafiki ambaye hatumfahamu sana, inaweza kuchukua muda zaidi kumtambua. Kadiri tunavyomfahamu Yesu, ndivyo tuwezavyo kutambua sauti yake. Anaweza kutumia njia mbili kuzungumza nasi

Mara nyingi Mungu anazungumza nasi tunapoomba. Tukiwa tunaomba, labda Mungu anaweza kutusababisha kukumbuka sana mtu fulani, na tunafikiri ‘labda anaumwa. Niende kwake kumtembelea’ Lakini ni lazima kupima mawazo



haya na Biblia (1 Jn 4:1). Tuone kama inafuata moyo wa Biblia. Je, inaonyesha upendo? Je, inatia moyo wakristo wenzetu, inaleta amani? Tukianza kufanya hivyo, je, tunasikia amani ya Mungu moyoni? (Kol 3:15)

Pengine Mungu anatupa ari ya kutaka sana kufanya kitu fulani. (Fil 2:13) Tunapoanza kumfahamu Mungu, pengine anafanya kazi miyoni mwetu kubadilisha tamaa zetu. Kwa mfano, labda mtu ataanza kutaka sana kuwa mchungaji. Mungu atampa moyo kufuata jambo hili na wazee wa kanisa na mchungaji wake mpaka atakapojuu kama kweli Mungu anataka awe mchungaji au sivyo.

## **Kutumia akili zetu**

Tunapokuwa wakristo, tunaitwa kutumia akili zetu. Mungu hajatupa ahadi yake tusiwe na kazi ya kutumia akili yetu. Kawaida Mungu atatuongoza kwa njia ya kutupa sababu ya kufanya mambo fulani. Tutumie akili kupanga shamba vizuri na kupata ushauri kuhusu mbegu mpya ili tupate mazao mazuri. Tujaribu kutazama mbele - ‘nikifanya hivyo, mambo fulani yatatokea - nisipofanya labda jambo fulani na fulani litatokea.’ Tutumie akili yetu kupanga njia zetu vizuri tunavyoweza. ‘Msiwe kama farasi wala nyumbu, walio hawana akili. Kwa matandiko ya lijamu na hatamu sharti kuwazuia hao, au hawatakukaribia’ (Zab 32:9)

## **Kupata ushauri wa wazee**

Mithali 12:15 ‘Yeye aliye na hekima husikiliza shauri’; Mithali 20:18 ‘Kila kusudi huthibitika kwa kushauriana’

LAKINI, mwishoni, kukata shauri ni kati yetu sisi na Mungu. Tukikosa, hatuwezi kumshitaki mwengine. Ushauri ni sehemu tu ya uongozi. Labda wengine wanaweza kutupa ushauri mbaya. Lazima tupime vyote pamoja.

Basi, tusikilize ushauri wa nani? Tunapaswa tuwaaulize wale tunaowaheshimu kwa sababu wanamfahamu sana Mungu. Heshima kwa Mungu ni mwanzo wa hekima, na tutumie watu ambao wanamheshimu Mungu, na wenyewe hekima na uzoefu mkubwa wa maisha. Labda pia ni wazo zuri kuwaauliza wazazi, kwa sababu wanatufahamu sana, na wanaweza kuona mambo fulani zaidi kuliko sisi. Tukizungumza na watu hawa kuhusu matatizo yetu, wanaweza kutusaidia kusikia sauti ya Mungu. Labda tuzungumze na watu mbalimbali, kupata mawazo mengine. Laki tusizungumze na watu wengi kabisa mpaka tutakapopata mtu anayekubali na tulivyotaka kufanya mwanzoni. Tusichague watu ambao watakulaliana nasi. Tuchague watu ambao tunawaheshimu katika Kristo, na tunaona kwamba wanaweza kutusaidia kumsikia Mungu mwenyewe.

## **Matukio**

Mungu anaweza kutawala matukio. (Mith 16:9) Mungu anaweza kufungua milango, na kuifunga (1 Kor 16:9, Mdo 16:7) Labda Mungu anatupa nafasi maalum kufanya kitu fulani, au anatuletea mtu anayebadilisha maisha yetu, wakati ule ule tulipohitaji. Au labda hatupati kwa mfano nafasi ya kusoma zaidi. Tunajaribu njia hii na nyingine, lakini wapi! Mungu amefunga mlango. Baadaye, pengine utafunguliwa tena.


Katika maisha yetu, labda baadaye tutaweza kuona kwamba ingalileta matatizo makubwa tungaliweza kwenda mahali fulani, au kufanya kitu fulani. Au, labda hatutaweza kuona kwa nini mpaka tutakopofika mbinguni.

Pengine tunaitwa kuendelea kujaribu hata ingawa matokeo si mazuri. Tunahitaji kupima kila kitu pamoja ili kujua njia zetu.

## **Kukumbuka**

- ◆ Tusiwe na haraka. Ibrahimu alisubiri miaka mingi kupata mtoto kabla ya kuona mkono wa Mungu. Wakati aliposubiri, alijaribu kuharakisha mambo kwa kutumia njia yake mwenyewe, lakini, alileta matatizo makubwa tu. (Mwanzo 16 na 21) Mungu alikuwa na kazi ya kumtayarisha Ibrahamu kabla ya kumpa mtoto. Tumwamini Mungu kwamba anajua sana kuliko sisi.
- ◆ Tutakosa sote. Tunajaribu kuharakisha mipango ya Mungu. Tunafuata mawazo yetu na kuacha njia za Mungu, na tunaleta matatizo mengi. Lakini Mungu anaweza kutengeneza mambo upya. (Yoeli 2:25) Anachukua maisha yetu na kuweza kuyatengeneza kuwa kitu cha thamani sana - ikiwa tunampa maisha yetu afanye kazi yake ndani yetu.

Rum 8:28. Tukifanya sehemu yetu - kusoma (Biblia), kusikiliza (Roho Mtakatifu), kufikiri (kutumia akili), kuzungumza (na wazee), kuangalia (matukio) na kusubiri, Mungu anaweza kufanya kazi nasi ili maisha yetu yawe mazuri mbele yake. Ni kama mtoto kujaribu kuchezea chombo cha muziki - baba yake anaweza kukaa naye na kucheza naye, na kubadilisha muziki wake kuwa mtamu sana.



## **Maswali**

1. Tunatumia njia gani kuamua kuhusu mambo katika maisha yetu?
2. Nini kinatuzuia kupokea mwongozo wa Mungu katika maisha yetu?
3. Mungu anatumia njia gani kuongoza watu leo?
4. Akili inachukua nafasi gani katika kutafuta nia ya Mungu kwa maisha yetu?
5. Tutapataje mtu wa kutushauri?
6. Tufanye nini ikiwa tunajisikia kama Mungu hajibu ombi letu la kuongozwa naye?
7. Tufanye nini ikiwa tumebaribu maisha yetu kwa kutomsikiliza Mungu?

## **Kwa nini tuwaambie wengine?**

Watu wengi wanasema ‘Naweza kuwa mkristo mwenyewe bila kuwaambia wote’. Wanafikiri kwamba imani yao ni mambo ya siri.

Labda tumesikia mhubiri akisema ni wajibu wetu kueneeza Injili. Lakini kwa nini tufanye hivyo?

Kwanza, kwa sababu Yesu aliagiza. Mara 233 katika Agano Jipya na mara 54 katika Injili ya Mathayo peke yake, Yesu alisema ‘Nenda’ ‘Nenda mwambie Yohanna....’ ‘Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi...’ Mat 28:18 - 20

Pili ni kwa sababu watu wanahitaji kusikia. Tukienda jangwani na kukuta chemchemi ya maji, je, ni vizuri kuweka habari hii kama jambo la siri? Lazima tuwaambie wengine. Wengi siku hizi wanaskikia kiu. Wanajaribu kujijaza kwa kutumia bangi, au pombe, au kukimbilia wanawake wengi. Lakini, tunajua kwamba mtu mmoja tu anaweza kuropa maji ya maisha.

Tatu, ni kwa sababu ni habari njema. Tunataka kuwaambia wote. Mama akizaa mtoto, Baba atakimbilia kwa jirani zake wote na kuwaambia ‘Nina Mwana! Hataki kulificha.

Lakini, kuna hatari mbili. Ya kwanza ni kuambia kila mtu wakati wote. Tukifanya hivyo, watu watachoka na habari hii kabla hawajasikia vizuri. Tunahitaji kuwa rafiki kwanza, na kustahili haki yetu kuwaambia Injili. Hatari ya pili ni kotowaambia kwa sababu ya hofu. Tunaogopa kwamba watu watacheka, watatukataa. Tukitembea na Yesu, tutaweza kukwepa hatari hizi, kwa sababu tutajua nafasi nzuri maana ni kazi ya Roho Mtakatifu moyoni.

Kuna njia nne za kutumia kuhubiri Injili

## **Uwepo wetu (Presence)**

### **Mat 5:13 - 16**

Tunaitwa kuishi ulimwenguni, si katika mazingira ya Kikristo tu, lakini kuwapo katika mambo ya ulimwengu - siasa, elimu, muziki n.k. Lakini tunaitwa kuishi maisha mapya, tofauti kuliko mwenzetu, kama chumvi na mwanga.

Chumvi ina kazi ya kuzuia nyama, samaki n.k. ili isioze. Vivyo hivyo, sisi tunaitwa kukoleza jamaa yetu, kuwepo kuangalia haki ya walemaavu, wale wasio na nguvu, labda kwa kujiingiza katika mambo ya siasa, labda kufanya kazi binafsi na watu wanaohitaji msaada.

Pia turuhusu mwanga wa Yesu kuingilia kila tendo letu na kumpenda jirani yetu kama nafsi yetu. Watu wakijua kwamba sisi ni wakristo,

wataangalia jinsi tunavyoishi, na matendo yetu yatawaambia zaidi kuliko neno lolote. (1 Pet 3:1 - 2)

Lakini, tukiishi vizuri, bila shaka wakati wa kusema kitu utafika. Tutasemaje?

## **Kuwavuta (Persuasion)**

### **2 Kor 5:11**



Tunahitaji kuweza kuzungumza na watu kuhusu imani yetu. Tunahitaji kujua kwa nini tunaamini, na kuwaonyesha majibu katika Biblia. Mdo 17:2 - 4

Watu labda watakuwa na maswali mengine, kama 'Kwa nini Mungu wa Upendo anaruhusu watu kuteswa?', au 'Je, kuhusu Imani nyingine kama Uislamu?'. Wanahitaji kujibiwa, na ni wazo zuri la kufikiri kuhusu majibu ya maswali kama haya mapema, ili tukiulizwa tuwe tayari. Lakini, mara nyingi wanaauliza kama njia ya kukwepa kufikiri kuhusu Kristo wenywewe. Tujibu maswali yao, lakini, turudi baadaye katika mambo ya msingi.

## **Kutangaza (Proclamation)**

Hatuwezi sote kuhubiri vizuri, lakini sisi sote tunaweza kuwaambia watu matukio ya maisha yetu, na tunaweza kusema wote 'njooni muone' Tunaweza kuwaalika watu kwa Ibada maalum au kusikiliza mhubiri mzuri ili wasikie vizuri. Lakini ushahidi wa maisha yetu ni muhimu pia. Hawatasikiliza bila kuona ushahidi katika maisha yetu, na maneno na tabia yetu.

## **Kusali (Prayer)**

Mara nyingi, mtu akianza kuwa mkristo, anakuta kwamba mwingine ameomba kwa ajili yake. Tukitaka watu wawe wakristo, lazima tuombe. Yesu alipokuwa akihubiri, alisali pia (Mk 1:35 - 37). Tunahitaji kuomba Mungu afungue macho yao ili waone ukweli wa Injili.

Tunahitaji kusali kwa ajili yetu pia. Tunapoanza kuwaambia wengine, labda tutapata shida. Watu hawatafurahi sana. Shetani hatafurahi. (Mdo 4:29 - 31) Lakini ni muhimu sana tuendelee na kazi hiyo. Tukifanya hivyo, kwenye kizazi chetu, tutaona maisha mengi yageuzwe na furaha kubwa.

## **Ambatanisho**

### **Kuandaa ushuhuda**

Mapendekezo

a) Fanya ushuhuda mfupi

Lenga kutumia kama dakika 3 hivi, baada ya hapo, watu hawaendelei kusikiliza

b) Uwe ushuhuda wako mwenyewe

Usihubiri, epuka kutumia ‘sisi’ wala ‘wewe’, tumia ‘mimi’

c) Kristo awe kiini

Watu wanapaswa kumfuata Kristo, sio wewe!

d) Mpango

- Sema kidogo juu ya maisha yako ya zamani
- Jinsi ulivyomjua Yesu katika maisha yako
- Lipi la muhimu tangu umjue Yesu

e) Sasa andika kwa kirefu

Ni rahisi kuona udhaifu kama ushuhuda umeandikwa

## **Sala**

Bwana Yesu Kristo, najutia dhambi zangu

(Tulia kidogo kuomba msamaha kwa lolote linalokushtaki katika dhamiri yako)

Tafadhali unisamehe. Nayaacha yote yaliyo maovu.

Asante kwa kufa msalabani kwa ajili yangu ili nisamehewe na kuwekwa huru

Asante kwa kunisamehe na kunipa Roho wako. Nakupokea sasa Ee Bwana.

Nakukaribisha katika maisha yangu kwa njia ya Roho Mtakatifu kuwa nami milele

Asante Bwana Yesu. Amina

## **Maswali**

1. Utamjibu nini mtu anayesema kwamba imani yake ni jambo la siri?
2. Ina maana gani katika maisha yetu kuwa chumvi na mwanga kwa wale wanaoishi pamoja nasi?
3. Tunawezaje kuwa na majibu mazuri kwa wale wanaouliza maswali kuhusu imani yetu?
4. Kusali ni muhimu katika kazi ya kuwaambia wengine habari njema. Kwa nini?
5. Tufanye nini ikiwa watu wanatucheka au kutufukuza kwa sababu ya imani yetu?
6. Tunawezaje kuleta watu kwake Yesu?

## **Je, Munqu anaponya leo?**

Tunasakiia habari nyingi siku hizi kuhusu watu ambao wameponya chini ya uinjilisti mbalimbali. Wakati mwingine, tunawaombea watu kanisani; ipo katika Ibada ya Ushirika Mtakatifu - 'waponye wagonjwa...'. Lakini je, tunaamini kwamba Mungu anaponya watu leo, hasa tunapokuwa na madaktari na wataalam wengine? Kazi ya kanisa iwe nini katika mambo haya?

### **Uponyaji katika Agano la Kale**

Tangu mwanzo, Mungu ameahidi kuleta afya na uponyaji kwa watu wanaomtii (Kut. 23:25 - 26, Kum 28). Ndiyo, ni mojawapo ya sifa zake - 'Kwa kuwa Mimi ndimi Bwana nikuponyaye' (Kut 15:26)

Katika Agano la Kale, kuna mifano mingi ya uponyaji wa Mungu, (Hes 21:9, 2 Fal 4:18-37, Isa 38-39) Tutazame habari ya Naamani (2 Wafalme 5), aliyekuwa na ukoma. Alikwenda kutafuta mtumishi wa Mungu, Elisha, pale Israeli na kuomba msaada wake. Mungu alimponya alipooga mara saba katika mto wa Yordani. Katika habari hii tunatambua kwamba uponyaji wake ulileta imani kwa Mungu - alianza kumwamini Mungu wa Israeli. Kama Mungu amefanya hivyo katika Agano la Kale, tena kwa watu wa nchi za kigeni, kwa nini tusimwamini kwamba afanye hivyo sasa wakati wa Agano Jipya?

### **Huduma ya Yesu**

Yesu alihubiri sana 'Ufalme wa Mungu' katika Injili. Maana yake si kwamba kuna mahali maalumu chini ya Mungu, tutakapofika baadaye. 'Ufalme wa Mungu' ni sawasawa na 'Utawala wa Mungu'.



Katika mafundisho ya Yesu, Ufalme wa Mungu una sura ya wakati ujao. Katika mfano mmoja Yesu alifundisha kuhusu mavuno yatakayotokea siku ya Mwisho. ‘Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, na kuwatupa katika tanuru la moto.....Ndipo wenyе haki watakapong’aa kama jua katika ufalme wa Baba yao (Mat 13:24-30, 36-43)’ Historia itafika kilele chake atakaporudi Yesu mara ya pili. Itakuwa mwisho wa ulimwengu huu. Wafu watafufuka na kila mtu atahukumiwa. Kwa wengine itakuwa siku ya upotevu; kwa wengine, watapewa urithi wao katika ufalme wa Mungu (Mat 25:34) Kutakuwa na mbingu mpya na nchi mpya. (Ufu 21:1) Wale waliompenda Yesu wataishi naye daima. Patakuwa mahali pa furaha kubwa. (1 Kor 2:9) Tutakuwa na miili yenye fahari ambayo haitaharibika (1 Kor 15:42 - 43) Hakuna mauti tena, wala maumivu, wala machozi (Ufu 21:4) Wale walioamini wataponywa kabisa siku ile, na kuishi katika uzima wa milele.

Lakini sura nyininge ya Ufalme wa Mungu ni kwamba ‘upo na umeshaanza’. ‘Yesu alipoulizwa na Mafarisayo, ‘Ufalme wa Mungu utakuja lini?’ alijwajibu akawaambia ‘Ufalme wa Mungu hauji kwa kuuchunguza; wala hawatasema Tazama uko huku, au kule, kwa maana, tazama, Ufalme wa Mungu umo ndani yenu’ (Lk 17:20-21) Alionyesha ishara kwamba ufalme umefika kwa matendo yake - kusamehe wenyе dhambi, kuponya wagonjwa, kutoa pepo, viwete kutembea, vipofu kuona - yote yanaonyesha utawala wa Mungu katika ulimwengu huu.

Kwa hiyo Ufalme wa Mungu ni ‘sasa’ na ‘bado’ Wayuhudi walifikiri kwamba Masihi ataleta ufalme kamili mara moja, na kutawala kabisa duniani kama mchoro chini unavyoonyesha.

---

SASA

ZAMANI IJAYO

---

Lakini Yesu alifundisha kwamba tunaishi katika wakati wa katikati. Ufalme wa Mungu umeanza lakini haujakamilika bado. Bado nguvu ya Shetani katika ulimwengu huu inaendelea, mpaka siku ile Yesu anaporudi kumaliza mambo. Kwa hiyo, wakati huu tunaendelea kuumwa, lakini Ufalme wa Mungu upo pia na ana uwezo wa kuingia katika hali hiyo na kutuponya.

Kuja kwake Yesu  
mara va kwanza

Kipindi ambacho  
tunaishi sasa

Kuja kwake Yesu  
mara va pili

## SASA

Robo ya Injili ni habari mbalimbali kuhusu watu walioponywa na Yesu. Tena Yesu aliwatuma wanafunzi wake waende wakafanya hivyo (Tazama Mat 9:35 - 10:15). Alituma kikundu cha watu sabini na wawili kuhubiri ufalme na kuponya watu (Lk 10:1 - 20) Kabla ya kupaa mbinguni, aliwaagiza 'Enendeni ulimwenguni mwote, mkahubiri Injili kwa kila kiumbe. ...Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;.....wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya. (Mk 16: 15 - 20) Na mara nyngi katika Matendo ya Mitume, tunaambibiwa habari ya watu walioponywa na wanafunzi na waaminio wengine (Mdo 3:1- 10, 4:12, 5:12 - 16, 8:5 - 13, 9:32-43, 14:3, 8-10, 19:11-12, 20:9-12, 28:8-9) Hata katika historia ya kanisa baadaye, kuna habari nyngi ya watu waliopona , kwa mfano Iraneus (140 - 203BK), Origen (185 - 254 BK), na Augustine (354 - 430 BK) Kwa hiyo, kuponya watu ni ishara moja ya Ufalme wa Mungu, na tunaweza kutazamia kwamba itaendelea mpaka siku yake ya kurudi Yesu mara ya pili. Hakuna sababu kwa nini isiendelee.

## Tuombeeje wanaoumwa?

Mungu anapoponya leo, inaturuhusu tuonje utamu wa wakati ujao, tutakapoona ukombozi wa mwili wetu (Rum 8:23) Lakini si kila mtu tunapomwombea atapona. Mara nyngi Mungu anatumia madaktari na wataalam wengine, na dawa mbalimbali. Na mara nyngine, inafaa zaidi kumwandaa mtu kwa kifo chake, au kumsaidia kuishi na ugonjwa wake, badala ya kuomba uponyaji wake. Tunahitaji kusali kufuata uongozi wa Roho Mtakatifu, na atatuonyesha nini na lini tuombe.

Hata tusipoona matokeo, watu wanapenda kuombewa. Inawaonyesha upendo na huruma ya Mungu katika hali zao. Tukiomba kwa huruma na hisia, watasaidiwa, hata wasipopona wakati huo huo.

Tunaagizwa tuwaombee wagonjwa, na ni maagizo kwa kila mkristo. Kama wengine wana kipawa cha uinjilisti, lakini wote wanaagizwa kutoa ushuhuda wa imani yao. Vivyo hivyo, wengine wana kipawa maalumu cha kuwaombea wagonjwa, lakini wote wanaweza kuomba.

## **Tunafanyaje?**

*Wapi panaumwa?* Tunauliza mgonjwa tatizo ni nini, na tuombée nini.

*Kwa nini mgonjwa ana hali hii?* Mara nyininge, sababu zaweza kuwa wazi - kwa mfano amegongwa na gari. Lakini, wengine wanaumwa kwa sababu ya wasiwasi, au matatizo nyumbani. Tuombe Mungu atuonyeshe kama kuna tatizo lingine nyuma ya hili linaloonekana

*Naomba vipi?* Kuna mifano mbalimbali katika Biblia, lakini yote ni rahisi. Tunaomba Mungu amponye mgonjwa. Pengine, tunasali pamoja na kupaka mafuta (Yak 5:14) Au Mara nydingi ni pamoja na kuweka mikono (Lk 4:40) Lakini bila msukosuko mkubwa, wala sauti ya juu, ila kuomba kwa upole na makini. Si ombi letu, bali nguvu ya Mungu inayoleta uponyaji

*Wao wanafanyaje?* Tunawauliza wanajisikiae. Mara nyininge, wanajisikia afadhali mara moja. Mara nyininge, hawasikii matokeo yoyote. Tunaendelea kuomba mpaka tunajisikia inatosha.

*Hatua gani inafuata?* Tunahitaji kuwatia moyo watu kwamba Mungu anawapenda, kama wamepona au sivyo. Tunaweza kurudi na kuomba tena wakati mwengine. Tusiwaambie watu kwamba hawajapona kwa sababu hawana imani - Haiwezi kuwa kweli. Mungu hafanyi kazi hivyo, na unamwongezea mgonjwa mizigo mikubwa ya hatia. Tunawatia moyo watu waendelee kuomba, na hasa wakae katika jamii ya kanisa - ndipo mahali ambapo uponyaji wa mwili na roho pamoja unaendelea kutokea mara nydingi. Imani zao hujengwa na kukua kwa njia hiyo ya kuwatia moyo badala ya kuwakatisha tamaa.

## Maswali

1. Ufalme wa Mungu ni 'sasa' na 'baadaye'. Hii ina maana gani? Inatusaidiaje tunapofikiri kuhusu uponyaji?
  2. Si kila mtu tunayemwombea atapona. Kwa nini? Ina umuhimu gani?
  3. Kwa nini ni muhimu kuwaombea wagonjwa? Kwa nini tunaogopa?
  4. Tuombe kwa upole na makini. Kwa nini?

# Kanisa ni nini?

Je, Kanisa ni nini? Ukitsemu neno 'kanisa', watu wana mawazo mbalimbali. Wengine wanafikiri ni jengo. Wengine wanafikiri ni kazi ya makasisi wanayoifanya kila jumapili. Wengine wanafikiri ni wajibu wao kwenda kanisani, labda kwa pasaka, na ndoa, au jumapili nyingine; ni wajibu wao, kama ni wajibu kuwasalimu wazee, au kuchimba shimo la takataka. Biblia inatumia mifano mitano ya kanisa, kutusaidia kuelewa kanisa liliivyo.



## 1. Kanisa ni watu wa Mungu

Kanisa ni watu. Neno la Kigiriki kwa kanisa ni ekklesia - yaani, mkusanyiko wa watu. Ni wale wote duniani kote wanaokiri jina la Yesu Kristo.

Ubatizo ni alama inayoonekana kwa ulimwengu kwamba mtu ni mshiriki wa kanisa hili. Maana yake kuoshwa dhambi (1 Kor 6:11), kufa na kufufuliwa na Kristo ili kuishi maisha mapya (Rum 6:3 - 5, Kol 2:12), na maji yaliyo hai aliyoaleta Roho Mtakaifu katika maisha yetu (1 Kor 12:13, Yoh 7:37 - 39)

Kanisi hili ni kubwa. Lina washiriki wapatao milioni 1,700 katika nchi 254. Tunasoma katika Biblia kuhusu makanisa yaliyokuwapo sehemu mbalimbali wakati wa Agano Jipyä; kuhusu ongezeko la makanisa hayo, na vikundi vipyä vya wakristo vilivyopandwa mahali pengine.

Sisi pia tunakusanya pamoja kama watu wa Mungu katika vikundi mbalimbali. Wakati fulani makanisa yanakusanya pamoja kwenye mkutano mkubwa kabisa, kama vile maadhisho ya sikuu, au mafundisho maalum. Tena, huwa tunakusanya kila jumapili kwenye vikundi vidogo zaidi kwa Ibada ya kawaida. Na pengine tunakusanya pia kwenye vikundi vidogovidogo nyumbani kusoma Biblia, kuombeana n.k. Vikundi hivi vyote ni muhimu.

Tunapokusanya wengi, tunatiwa moyo sana. Twaona nguvu ya Mungu, twamwabudu pamoja. Tunafundishwa na wataalam, na pia jamii yote inaweza kuona kwamba kanisa ni hai.

Tunapokusanya kila juma vijijiini, tunawafahamu wenzetu karibu wote. Tunaweza kutiana moyo kwa sababu ya urafiki wetu, na kufanya kazi pamoja vizuri. Tunaweza kujifunza kwa mfano kusoma somo mbele ya kanisa, kuimba kwenye kwaya, labda kuongoza Ibada au kuhubiri - tuna uhuru kwa sababu tunafahamiana na kupendana.

Ni vizuri pia kukusanya katika vikundi vidogovidogo, kwa sababu pale tunaweza kuombewa mambo ya siri zaidi, na tunaweza kueleza jinsi mambo yalivyo kweli, na mawazo yaliyomo miyonyo mwetu.

## **2. Kanisa ni familia ya Mungu**

Tunapompokea Yesu tunafanya kuwa watoto wa Mungu (Yoh 1:12) Hii inalipa kanisa umoja wake. Tupo familia moja. Ingawa kaka na dada wanaweza kubishana, hawawezi kuacha kuwa damu moja. Vile vile, ingawa kanisa linaonekana kwamba lina tofauti kubwa, bado tupo familia moja. Labda hatuoni kwamba ni rahisi kuishi na wakristo wenzetu kila wakati. Labda tutabishana, na hata kutaka kuachana. Lakini, kama familia ambayo imegawanyika, tujaribu kufanya kazi ili tusuluhihwe, na kuwa na umoja tena. Mara nydingi tunapomkaribia Mungu, tunawakaribia wenzetu pia. Tukibishana ni kama tunaweka ua kati yetu na wenzetu. Lakini tukipanda juu ya mlima, hata ua mkubwa utaonekana kama si mrefu mno. Tunapoinua miyoyo yetu kumwabudu Mungu, tofauti yetu inaonekana kuwa ndogo sana kuliko umoja wetu katika Yesu Kristo.

Tunaitwa kushirikiana. Huwezi kuoana peke yako, na vilevile, huwezi kuwa mkristo peke yako. Tunawahitaji wakristo wenzetu. 'Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimiziana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane, na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia' (Ebr 10: 24 - 25) Kipande kimoja cha mkaa peke yake kinaweza kupoa, lakini vyote pamoja vinabaki na joto. Tunahitajiana. Hatuwezi kuondoka katika familia yetu.

### **3. Kanisa ni mwili wa Kristo**

Sisi Wakristo tunamwonyesha Kristo kwa ulimwengu. Watu hawawezi kumwona Yesu, lakini wanatuona sisi - tufanyavyo, tusemavyo. Yesu anatutumia sisi kufanya kazi yake hapa duniani

Mtume Paulo anasema katika Wakorintho wa kwanza sura ya 12 kwamba kanisa ni mwili wa Kristo. Tupo kwenye mwili mmoja, lakini maana yake siyo kwamba sisi sote tunafanana kabisa. Tupo tofauti, kama sikio ni tofauti kuliko mguu. Mwili una sehemu nyingi, na sisi sote pia ni tofauti, wenye vipawa tofauti na kazi tofauti.

Paulo anasema mambo mawili hasa kuhusu mwili. Kwanza anasema kwamba hatuwezi kusema 'Mimi sihitajiwi. Si muhimu kama nipo au sipo.' Mwili unahitaji sehemu zote kufanya kazi yake vizuri. Kila mtu anahitajiwa kushirikiana katika maisha ya kanisa; la sivyo, kanisa litashindwa kufanya kazi yake vizuri, kama mwili wa kilema. Pili, hatuwezi kusema kuhusu mwiningine 'Simhitaji. Siye muhimu katika maisha ya kanisa'. Kusema hivi ni kama macho kusema 'sihitaji mkono'. Haiwezekani. Kila mtu ni muhimu katika kanisa la Kristo.

Tatizo moja la kanisa ni kwamba mara nyingi linaonekana kuwa kazi ya makasisi na makatekisti tu. Kwa sababu mtu hana kazi maalum kanisani, anaanza kusikia kama si muhimu kama yupo au hayupo. Yupo kama mtazamaji, sio kama mchezaji. Katika kanisa la Agano Jipyaa, kila mtu alishiriki katika Ibada, na kazi mbalimbali za kanisa. Sisi pia tunahitaji kumwingiza kila mtu katika kazi ya kanisa, kama vile kuwafundisha watoto, kupika chai, kusoma masomo, kuimba, kufanya usafi, kusikiliza shida za wenzake na kuwatia moyo - kuna kazi nyingi na tumsaidie kila mtu kujua wajibu wake.

### **4. Kanisa ni hekalu la Mungu**

Paulo anasema kwamba wakristo wanajengwa pamoja 'kuwa maskani ya Mungu katika Roho' (Efe 2:22) Kristo ni jiwe kuu la pemberi. Msingi ni mitume na manabii, na sisi kama mawe yaliyo hai tunajengwa pamoja kutengeneza hekalu takatifu.

Katika agano la kale, hekalu lilikuwa kiini cha Ibada ya Wana wa Israeli. Hapo palikuwa mahali walipokwenda watu kukutana na Mungu. Wakati fulani uso wa Mungu ulikuwapo kama wingu la moshi lililojaa hekaluni. Palikuwa na hema lililoitwa Patakatifu pa patakatifu, na Kuhani Mkuu tu aliweza kuingia, mara moja kila mwaka, baada ya kutoa damu kwa ajili ya dhambi zake na za watu wake.

Yesu alipokufa msalabani, alitufungulia njia ya kuingia Patakatifu pa

patakatifu anapokaa Mungu wakati wowote, mkristo yejote. Sasa Mungu hayupo katika mahali maalum, bali yupo na wakristo wote, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Hatuhitaji kuhani tena, bali kila mkristo anaweza kumkaribia Mungu. Kila mkristo anafanya kazi ya kuhani sasa; yaani kuwaleta watu mbele ya Mungu kwa maombi, na kumleta Mungu mbele ya watu kwa jinsi anavyoishi.

Tena, hatuhitaji kutoa dhabihu tena, kwa sababu Yesu alitolewa kama dhabihuu kamili mara moja kwa ajili ya watu wote na wakati wote. Tunaadhimisha hii katika Ibada ya Ushirika Mtakatifu. Ibada hii ni Ibada maalum, tunapochukua vitu tunavyoweza kuvigusa kutusaidia kuelewa mambo yasiyoonekana.

*Twatazama nyuma na shukrani:* Twakumbuka mwili wa Kristo uliovunjwa na damu yake iliyomwagika msalabani. Twakumbuka kwamba alikufa ili dhambi zetu ziondolewe, na tuweze kumkaribia Mungu, na tumshukuru.



*Twatazama mbele na tumaini:* Mara nyingi tunasherehekea sikukuu na mlo maalum. Mwishoni tunaalikwa kusherehekea katika karamu ya Arusi ya Mwana-Kondoo. (Ufu 19:9) Mkate na Divai inatukumbusha kwamba siku moja tutakaa Mbinguni na watakatifu wote hata milele.

*Twatazama pande zetu kwa familia ya kikristo:* Kwa sababu tunakula mkate mmoja, unatukumbusha kwamba sisi tu mwili mmoja. (1 Kor 10:17) Kula na kunywa hivyo kunatukumbusha umoja wetu. Tukiwatazama wenzetu, tunakumbuka kwamba ni kwa neema ya Mungu kwamba tunaweza kula mezani kwa Bwana - hamna mtu anayestahili. Tupo wote sawa sawa, na tunakuja kwa mwaliko wa Yesu mwenyewe

*Twatazama juu kwa matazamio:* Yesu anakutana nasi katika tendo la kushirikiana katika meza ya Bwana, kwa Roho Mtakatifu, na tunaweza kufurahia kwamba yupo pamoja nasi.

## **5. Kanisa ni Bibi Arusi wa Kristo**

Biblia inatumia ndoa kama mfano wa uhusiano kati ya Yesu Kristo na kanisa lake. Kwa mfano, waraka wa Waefeso, sura ya 5, mstari wa 25 - 27 unasema 'Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo alivyopenda Kanisa, akajitao kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa.'

Labda utafikiri kwamba hutambui picha hii ya kanisa la sasa hivi, lakini inatupa picha ya mpango wa Yesu kwa Kanisa lake na siku moja itatokea. Siku moja Yesu atarudi na utukufu, na tutaona 'Yerusalemu mpya, ikishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu, imewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe' (Ufu 21:2) Sasa hivi, kanisa ni dogo na dhaifu. Lakini siku moja litakuwa kama alivyopanga Mungu, linalofaa kuishi naye daima. Hata sasa hivi Mungu anaweza katuona kama tutakavyokuwa - ana huzuni kwa sababu ya makosa yetu, lakini pia anafurahia kujua kwamba tutakamilishwa kufanana naye.

Tukitazamia hivyo, tutajitahidi sasa hivi kuishi maisha matakatifu na safi, ili tuwe tayari atakaporudi tena, na kwa shukrani kwa jinsi atakavyotufanya. Hakuna Bibi Arusi anayesema 'Sihitaji kujipamba. Bwana Arusi atanichukua hata kama nilivyo' Anajitayarisha na furaha. Pia tutashangaa upendo wake na hatuwezi kukwepa kuwaambia wengine habari yake njema. Tutajaa furaha kwa sababu ya tumaini letu. 'Bali nyinyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpare kuzitangaza fadhili zake yeche aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu.' (1 Pet 2:9) Hii ndiyo sababu ya Kanisa - kumtukuza Mungu na kumfurahia daima.

Kanisa lingekuwa hivyo, tungekimbia pale kila Jumapili - na ingekuwa kama mbinguni hapa duniani. Hata sasa, tujifunze kuona na macho kama yale ya Mungu, na tutaona kanisa lake lapendwa, na tufurahi kufanya kazi naye ili likamilishwe kuwa Bibi Arusi anayemfaa.

## **Maswali**

1. 'Kanisa' - maana yake nini kwa uzoefu wako?
  
  
  
  
  
  
2. Biblia inatumia picha gani za kanisa? Ipi inakusaidia zaidi kuelewa zaidi kuhusu kanisa?
  
  
  
  
  
  
3. Tunaweza kufanya nini kuhusu mambo yanayotugawa sisi na wakristo wenzetu?
  
  
  
  
  
  
4. Huwezi kuwa mkristo peke yako - Je unakubali? Unahitaji wakristo wenzako kwa ajili ya nini? Wanakuhitaji kwa kazi gani?
  
  
  
  
  
  
5. Ukuhani wa wakristo wote. Una maana gani kwa maisha yetu ya kila siku?
  
  
  
  
  
  
6. Kwa njia gani kanisa letu silo kama linavyodhihirika katika Agano Jipya? Tunaweza kufanya nini ili kulibadilisha liwe nafuu kuliko sasa?

# Je, Naweza kuutumiaje vizuri muda wa maisha yangu uliobaki?

Tunapewa nafasi moja tu ya kuishi. Wengi tungetaka nafasi mbili - nafasi ya kwanza kujifunza kutokana na makosa yetu, na nafasi ya pili kufurahia! Lakini hatutapewa nafasi hiyo. Tunaishi mara moja tu.

Lakini, hata ikiwa tumefanya makosa mengi mpaka sasa hivi, inawezekana kutumia vizuri muda wetu uliobaki, na msaada wa Mungu. Tutafanyaje? Tufuate ushauri wa Paulo katika Warumi sura ya 12, hasa mistari ya 1 - 2. 'Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndivyo Ibada yenu yenyeye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.'

## Tufanye nini basi?

### Tusiifuatishe dunia hii

Paulo anasema 'Msiifuatishe namna ya dunia hii'. Tunaweza kujisikia kama tunabanwa na watu ambao wanatuzunguka, tufanane nao. Lakini tunapoanza kuwa wakristo, tuko tofauti sasa. Ni rahisi zaidi kufanana na watu wengine, kutoa sare rasmi na kuwa mtu wa kawaida. Lakini hatuitwi kuwa kigeugeu, ambaye anajibadilishia rangi kufanana na mazingira yake. Wakristo wengine ni hivyo - wanapokuwa pamoja na wakristo wenzao, wanaonekana kama wakristo wazuri. Wanaimba katika kwaya, wanaongoza Ibada vizuri sana. Lakini wakienda kazini au hotelini, wanabadilisha tabia zao kabisa. Wanajiunga na ulevi, au kuibaiba, wanatenda maovu kama wenzao wote wa pale. Mkristo kama huyu anaishi kwa kuhangaika sana - hawezи kufikia matokeo mazuri - kwa sababu anajaribu kufuata njia mbili kwa mara moja.

Tunaitwa kuwa tofauti na watu ambao wanatuzunguka - si katika mavazi yetu wala kusema lugha nyingine. Hatutakiwi kuonekana kama watu wa mzaha. Bali tuwe watu wakamilifu, kuonyesha ulimwengu jinsi Mungu alivyopanga binadamu aishi. Ikiwa ni hivyo, hatuwezi kuishi tena kama kawaida ya ulimwengu huu - kwa mfano kulalamika, kuibaiba, kujamiiiana na wenzetu. Badala ya hivyo, tuonyeshe kinyume chake, yaani moyo ya furaha, uaminifu, mustarehe na furaha ya ndoa ya kikristo.

Jambo la mwisho hili, kutojamiiiana kabla ya ndoa, ni jambo gumu kwa wakristo wengi. Tutazame kwa ukaribu zaidi.

Kwanza, Mungu alituumba kama watu watakaofurahia na kukutana

kimwili. Katika Wimbo ulio Bora, Biblia inashangilia kipawa hiki.

Lakini, aliyekiumba anatushauri kuhusu matumizi yake bora. Kama inavyosema katika Mwanzo 2:24 ‘mwanaume atamwacha baba yake na mama yake, naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja’ Ndoa ni kufanya tendo mbele ya jamii la kuacha wazazi na kuahidi kuishi maisha yote na mwenzako. Unaunganishwa na mwenzako kama kutumia gundi - si kimwili tu, bali kiroho, kwa kutegemeana, katika furaha na huzuni. Ni kitu imara sana katika kujenga jamii na kulea watoto wenye mwanzo mzuri, pia kwako kujengana na mwenzako anayekupenda na kututunza, na kuishi maisha mema pamoja naye.

Lakini tukijamiiana oyoovyo, tunavunja mpango huu wa Mungu. Kila tunapojuunga na mwingine, tunafanywa mwili mmoja. Unapovunja muungano huu, watu wanaumwa. Ukiunga karatasi mbili na gundi, huwezi kuzigawa tena bila ya kuacha kipande kidogo cha ukurasa mmoja katika ukurasa mwingine. Tukijiunga mwilini na mwingine, hatuwezi kugawanywa tena bila ya kuacha kipande cha maisha yetu katika muungano uliyovunjika. Tukitazama jamii yetu, tunaona ndoa zinazovunjika, watoto wanaozaliwa bila ya kutakiwa, magonjwa ya zinaa, na maisha ambayo yameharibika. Ni kweli, Mungu anaweza kurekebisha mambo, lakini yanaacha majeraha yao maishani mwetu, na ni afadhalii kuepuka hali hiyo.

Hata ukipanga kumwoa mwenzako baadaye na unataka kukutana kimwili kwanza, hii inavunja mpango wa Mungu pia. Yoyote yanaweza kutokea inayovunja mipango yenu. Mwenzako akipata mimba, labda wazazi wanaweza kumkataa. Labda mmoja wenu atavutwa na mwingine - maana hamjaahidi kuwa waaminifu bado. Labda tatiozo lingine linaweza kutokea. Lazima kusubiri mpaka ndoa - mkishaahidiana mbele ya jamii kwamba nyinyi mtaishi pamoja mpaka kufa, hakuna sababu kuogopa tena. Hii ndiyo nafasi iliyosahihi kufurahiana katika usalama na ukamilifu

Kwa hiyo tusiifuatishe dunia hii; bali tuwaonyeshe njia njema. Mwanga uking’aa watu watakuwa kuona kung’aa kwake.

## tugeuzwe....

Paulo anasema tugeuzwe kwa kufanywa upya nia zetu. Tuwe kama buu linalobadilishwa kuwa kipepeo. Tusiogope mabadilisho haya - yanaleta furaha na mema.

Tunaitwa kuacha mambo yote yanayoharibu maisha yetu, tuyaone kama takataka. (Fil 3:8) Kwa mfano inaweza kuwa kawaida mbaya, au urafiki mbaya. Badala ya haya, lengo letu liwe kuishi pamoja kama ilivyoandikwa katika mistari inayofuata katika Warumi 12 (mst 9 - 21) - kuonyesha upendo wa kweli, juhudhi katika Bwana, ushirikiano katika familia ya kikristo. Hii ni picha nzuri inayonyesha maana ya kuishi pamoja kama familia ya kanisa.

## Itoeni miili yenu...



Hili ni tendo la nia. Tunaamua kujitoa. Si kila wakati tutakuwa na hamu ya kufanya hivyo, lakini, tukiamua kuifanya, tutaifanya bila kusikiliza sana hisia zetu. Hizi zitafuata baadaye.

Tutoe –

muda wetu Tunahitaji kumpa Mungu nafasi katika maisha yetu - kusoma Biblia na kusali, kuwasaidia wengine, kuwatia moyo wengine n.k.

matakwa yetu Si kosa kutaka kuijendeleza, lakini bei yake isiwe kuacha kumfuata Mungu, na kusahau kuendeleza Ufalme wa Mungu kwanza (Mat 6:33)

fedha na mali zetu Tusijifikiri sisi wenyewe kwanza, lakini tuwe tayari kutumia mali yetu kwa maendeleo ya Ufalme wa Mungu hapa duniani, na kutoamini mali yetu kwamba itatupatia maisha yenyeye raha

masikio Tuache kusikiliza maongezi mabaya, muziki mbaya, kila kitu ambacho kinatuvuta kwenye njia mbaya

macho Tunachoona kinawenza kuleta majoribu ya wivu, au tamaa mbaya. Tuanze kawaida ya kuwatazama watu na macho ya Mungu - kufikiri 'nitawezaje kuwa baraka kwa huyu?'

midomo Midomo yetu ina nguvu ya kuwajenga watu au kuwaharibu. Tunaweza kuitumia kudanganya watu, au kuwatia moyo. Tuangalie jinsi tunavyozungumza, ili tuwe na maneno yanayoleta maisha mazuri.

mikono Tunaweza kutumia mikono kujijenga sisi na wengine, au kufanya matendo mabaya.

Hatuwezi kuchagua baadhi ya mambo ya kufanya. Tunaitwa kutoa mwili mzima kumtumikia Mungu. Lakini tunakuta kwamba tukijitoa kabisa, tutapata uhuru kamili. Hatutajisikia kama watumwa, bali kama tunaishi maisha makamilifu

### **.Kama dhabihu**

Kufanya hivyo haitakuwa bila gharama yake. 'Yesu hakuja kurahisisha maisha, bali kuwfanya watu kuwa wenye nguvu' Haitakuwa rahisi kuwa watu tofauti kuliko wenzetu, kwa kuishi vizuri katika ulimwengu wa dhambi. Wengine watafukuzwa na familia, wengine watateswa sana. Wengine watachekwa na marafiki. Wengine watahitaji kurudisha mali ambayo wameiba, au kuacha kazi ambayo hawawezi kuendelea kufanya.

### **.Kujua mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu**

Mungu anatupenda na anatutakia mema kwa maisha yetu. Shetani anaitwa 'msingiziaji', na anapenda sana kusema uwongo kuhusu Mungu 'Mungu hajui maisha ya kisasa. Haelewi jinsi mambo yalivyo sasa' au 'ataondoa furaha yote. Tunahitaji kutumia nguvu zetu zote katika kuishi maisha safi, bila kufurahishwa' Huu ni uwongo. Je, kuna Baba mzuri, ambaye ikiwa mtoto wake anasema 'leo, Baba, nataka kukufurahisha kwa sababu nakupenda', yeye akasema 'Basi, itanifurahisha sana kukufungia kwenye kabati kwa siku nzima'?

Nia yake Mungu kwetu sisi ni ukamilifu - hatuwezi kupata mema zaidi katika kufuata njia zetu sisi wenyewe. Tusidhani kwamba tunajua zaidi kuliko Mungu, la hasha! Yeye anajua mwanzo na mwisho, na anatupenda kama watoto wake. Tukimwamini, tutaanza kuona kwamba mapenzi yake ni ukamilifu kwetu. Jaribu, na uptaona!

Tumalize na Waebrania 12:1- 2. 'Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi

mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. Mtafakarini sana..msije mkachoka mkizimia moyoni mwenu'

Tukimtazama Yesu, tutaona upendo wa Mungu. Haiwezekani kutomwamini 'Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye' (Rum 8:32) Hisa yetu katika kuishi maisha ya Kikristo ni upendo wa Mungu. Ni mfano wa Mwana. Tunaishi katika nguvu ya Roho Mtakatifu. Tusichoke kumfuata, na kumpenda na kumtumikia. Ni maisha yaliyo mema kuliko yote, ni heshima na furaha kubwa.

## Maswali

1. Kwa njia gani tunabanwa na wenzetu wa ulimwengu ili tufanane nao? Kwa nini? Tunawezaje kusimama imara na kuishi maisha tofauti?
2. Kukutana kimwili kufanikiwe katika hali ya sharti la maisha mazima kati ya mwanaume mmoja na mwanamke mmoja katika ndoa ya kikristo tu. Kwa nini iko hivyo? Kuna hatari gani katika kuvuka mipaka hii?
3. Tuache nyuma takataka katika maisha yetu. Hii ina maana gani kwa kila siku?
4. Tutajuaje mambo yaliyo na umuhimu zaidi katika maisha yetu?
5. Imani yetu inaweza kuleta dhabihu. Umeona hii? Je, ina thamani gani mbele yako?
6. Ina maana gani kumtazama Yesu? Itatusaidiaje kuishi maisha ya Kikristo?